**Walichoteta** upinzani na Naibu Waziri Marekani, salamu za Samia zafika

UKURASA 7



**Canada** yatoa bil. 8.6/- kuchangia mpango wa serikali hifadhi ya jamii

UKURASA 4





# Nipashe

Ijumaa Agosti 6, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580664

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


BIASHARA

## Vijana wajipanga kupigania uchumi kupitia mlango wa bidhaa usindikaji

● YPC kijana njia za 'pa kutokea'

Na Julieth Mkireri, KIBAHA



UKURASA 11



# KESI YA MBOWE
# HAIJAPATA KUTOKEA

UKURASA 2

Mashtaka sasa kubadilishwa, UN yapeleka waangalizi kortini, mtandao wakwamisha kusikilizwa, majaji wanne kuamua shauri lake kikatiba... Uk. 2& 4









Matukio mbalimbali yanayoonyesha askari Polisi, wakikabiliana na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), waliofika katika eneo la jirani na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, kufuatilia kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Freeman Mbowe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ukiwa kundi hili usichanje mpaka ushauri wa daktari

UKURASA3



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wapili kulia), akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Sanlam, Julius Magabe (wapili kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa Strategis, Dk. Flora Minja (kulia), Mkurugenzi Mkuu wa Alliance Life, Byford Mutimusakwa (kushoto) na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa (katikati), wakionyesha vifaa vitakavyotumika katika mbio za kimataifa za 'CRDB Bank Marathon', jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kachero: Sabaya alitoa kichapo

UK.3

**MICHEZO** **WAFURIKA USAJILI CRDB BANK MARATHON** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# ...Ulinzi Dar, Mwanza, 11 watiwa mbaroni

**Na Waandishi Wetu**

MAGARI ya doria yenye askari polisi waliovalia sare wakiwa na silaha za moto zikiwamo bunduki, mabomu na mbwa jana yalipiga kambi nje ya ofisi za Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Victoria. Wakati hayo yakiendelea Mwanza, jijini Dar es Salaam Jeshi la Polisi jana lilikuwa likiwakamata watu 11 waliodaiwa kwenda katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakiwa na mabango.

Jijini Mwanza Nipashe ilishuhudia askari polisi wakizizunguka ofisi hizo za kanda kuanzia saa nne asubuhi huku wakiwa wanatazama ndani ya ukuta wa ofisi hizo bila kushuka kwenye magari yao.

Msafara wa magari takribani saba ulipita mara kadhaa katika ofisi hizo huku ndani kukiwa na wanachama wachache pamoja na viongozi wa CHADEMA waliokuwa wamekaa nje ya ofisi hizo. Baada ya kuzunguka muda mrefu, magari hayo yenye askari yaliegeshwa pembezoni mwa barabara umbali wa mita takriban 100 kutoka ziliko ofisi za chama hicho, lakini muda wote mpaka mchana hakuna askari polisi aliyeshuka na kuingia katika ofisi hizo.

Baadhi ya wanachama waliokutwa na Nipashe katika ofisi hizo, walisema hawawezi kuwakimbia polisi kwa kuwa hakuna kosa walilolitenda.

Licha ya kuwapo magari hayo ya polisi yaliyokuwa yakizunguka ofisi hizo, wanachama hao walitulia na kufanya walichokiita maombi maalum ya kuliombea taifa pamoja Mwenyekiti wao, Freeman Mbowe.

Maombi hayo yaliendeshwa na Makamu Mwenyekiti wa Makanisa ya Kikristo mkoani Mwanza, Askofu Amosi Hulilo.

Katika maombi hayo yaliyochukua takribani dakika 20, Askofu Hulilo alisema hakuna mtu yeyote mwenye akili anayeweza kupigana na upepo bali anaweza kupigana na mtu ambaye ana kitu fulani ndani yake. Alisema maombi hayo yalilenga kuwaombea viongozi mbalimbali wa kisiasa akiwamo Mbowe na taifa kwa ujumla.

Askofu Hulilo alisema mtu anayekimbia peke yake mara nyingi hapati ushindi bali anayetembea na wenzake anafanikiwa kushinda.

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Ilemela jijini Mwanza, Mbutusyo Mwakalaba, alisema jana walikutana ofisini huko ili kufanya maombi maalum kwa ajili ya taifa pamoja na kumwombea mwenyekiti wao (Mbowe).

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Zakaria Obadi, alisema hakuna mwanachama wao aliyekamatwa na polisi.

Hata hivyo, alisema wamepata taarifa wanatafutwa ingawa hawajajua makosa yao na kwamba leo pia wataendelea na maombi yao yanayomhusu Mbowe.

■**Imeandikwa na Richard Makore (MWANZA) na Romana Mallya (DAR)**




MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **FNB Bank Tanzania Limited, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunamtangazia mdaiwa au mteja wa benki tajwa hapo juu kulipa mkopo wake ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili kwenye gazeti. Kushindwa kufanya hivyo kutapelekea sisi kuuza dhamana ya mdaiwa aliyoiweka benki wakati anachukua mkopo kwa njia ya mnada wa binafsi (Private Sale). Mnada utafanyika mahali nyumba/dhamana iliko kama inavyoonesha hapa chini kwenye jedwali.

| S/N | JINA LA MTEJA/MDAIWA | AINA YA DHAMANA | DHAMANA MAHALI ILIKO | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | TANZANIA SPRING INDUSTRIES AND AUTO PART LIMITED | FIRST CHARGE LEGAL MORTGAGE RESIDENTIAL PROPERTY TITLE NO. 19453, PLOT NO. 40, KUNDUCHI BEACH AREA, KINONDONI MUNICIPALITY IN DAR ES SALAAM CITY | KUNDUCHI BEACH | 20/08/2021 SAA: 05:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei ya mnada mara baada ya nyundo ya dalali kutua.
2. 75% inayobaki itatakiwa kulipwa ndani ya siku 14.
3. Gharama za kuhamisha umiliki wa dhamana ni za mnunuzi
4. Dhamana itauzwa kama ilivyo

MAWASILIANO +255 765 999 000 AU +255 787 288 442




Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi Taifa, James Mbatia (wapili kushoto), akijadiliana jambo na Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika (kulia), katika viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, walipofika kufuatilia kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA, Freeman Mbowe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Haijapata kutokea kesi ya kina Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

WAFUASI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), jana walifurika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam kushuhudia usikilizwaji wa kesi inayomkabili mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe.

Hata hivyo, wengi wao hawakufanikiwa kuingia baada ya askari waliozingira mahakama hiyo kuwazuia nje ya ukuta.

Baadhi ya wafuasi hao walikuwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali yaliyoonekana kuilenga kesi hiyo ambayo jana ilikuwa inatajwa mahakamani huko.

Kesi hiyo iliendeshwa kwa njia ya Mahakama Mtandao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, mshtakiwa Mbowe na wenzake hawakupelekwa mahakamani, hivyo walisikiliza kesi wakiwa Gereza Kuu Ukonga.

Viongozi wa CHADEMA akiwamo Katibu Mkuu, John Mnyika, Joseph Mbilinyi 'Sugu', Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia na waangalizi wa kimataifa wanne kutoka Umoja wa Mataifa (UN) na Ubalozi wa Sweden nchini walifanikiwa kuingia kwenye ukumbi maalum wa Mahakama Mtandao.

Mawakili wa Serikali, Pius Hillary, Christopher Msigwa na Grace Mwanga waliiwakilisha Jamhuri huku washtakiwa wakitetewa na mawakili Peter Kibatala, John Mallya na Fredrick Kihwelo.

Wakati anaingia mahakamani majira ya saa 12 asubuhi, Wakili Kibatala alionekana akivuta begi lake lililosheheni vitabu na nyaraka za kisheria.

**KUBADILI MASHTAKA**

Wakili Hillar alidai washtakiwa wote wanaonekana wapo, kesi ilikuja kwa kutajwa na wanaomba kubadilisha hati ya mashtaka.

Wakili Kibatala hakuwa na pingamizi kwa washtakiwa kusomewa mashtaka mapya, hivyo Hakimu Simba aliwafahamisha washtakiwa na kuwauliza kama wanasikia vizuri au la.

Washtakiwa kwa pamoja walidai wanasikia sauti, lakini hawaoni picha ya mahakama iliyoketi kwenye Ukumbi wa Kisutu.

Hakimu Simba aliwafahamisha kwamba Mahakama ya Kisutu inawaona na kuwasikia vizuri, aliamuru warekebishe mtandao ili washtakiwa waione mahakama.

Marekebisho yalifanyika kwa zaidi ya nusu saa lakini washtakiwa hawakufanikiwa kuiona mahakama.

Wakili Hillar alidai kutokana na matatizo ya mtandao wanaomba washtakiwa wapelekwe mahakamani leo ili wasomewe, hoja iliyokubaliwa na Upande wa Utetezi.

Hakimu Simba baada ya kusikiliza hoja hizo, aliamuru washtakiwa wafikishwe mahakamani leo, hati ya kuwapeleka iwasilishwe gerezani.

Mbowe alifikishwa mahakamani Julai 26 na kuunganishwa na washtakiwa Halfan Hassan, Adam Kasekwa, maarufu Adamo na Mohamed Lingwenya, ambao walishasomewa kesi ya uhujumu uchumi namba 63/2020.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita. Katika shtaka la kwanza, wanadaiwa kula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi 2020 katika Hoteli ya Aishi iliyoko Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kutenda vitendo vya kigaidi kwa kulipua vituo vya mafuta.

Katika shtaka la pili, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali huko, aliwawezesha kifedha Halfani, Adamu na Lingwenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi kwa kutengeneza milipuko na kupanga kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na mikutano ya hadhara kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Tanzania.

Katika shtaka la tatu, washtakiwa Halfani, Adamu na Lingwenya wanashtakiwa kwa kupokea fedha hizo kutoka kwa Mbowe.

Mshtakiwa Adamu, katika shtaka la nne, anadaiwa Agosti 5, 2020, eneo la Rau, alikutwa na bastola yenye namba A 5340 aina ya Luger bila kuwa na kibali.

Katika shtaka la tano, mshtakiwa Adamu anadaiwa siku na mahali huko, alikutwa na vilipuzi ambavyo ni risasi tatu bila ya kuwa na leseni.

Mshtakiwa Halfani anadaiwa Agosti 10, mwaka 2020, kwa lengo la kuhatarisha usalama wa nchi, alitumia sare za Jeshi la Wananchi (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kinyume cha sheria.

Vifaa anavyodaiwa kuvitumia ni suruali moja ya JKT, suruali nne za JWTZ, fulana moja, koti la mvua moja, jaketi moja, kofia tano, overall tano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja, sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote vya JWTZ.

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TBL Plc, Cleopa Msuya (katikati), akifungua mkutano wa mwaka wa 48 wa wanahisa wa kampuni hiyo, uliofanyika kwa njia ya mtandao, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa TBL, Jose Moran na Mkurugenzi aliyemaliza muda wake, Philip Redman. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukiwa kundi hili usichanje mpaka ushauri wa daktari

**Na Mwandishi Wetu**

JOPO la wataalamu wa afya wa mashirika ya Kimarekani nchini, limetaja makundi matatu ya watu ambao hawastahili kuchanjwa chanjo ya Uviko-19.

Makundi hayo yametajwa kuwa ni wenye umri wa chini ya miaka 18, anayejisikia kuumwa kama homa siku anayotakiwa kuchanjwa na wenye mzio (allergic), huku wajawazito, wenye ugonjwa wa kifua kikuu na upungufu wa damu wakitakiwa kupata ushauri wa madaktari kwanza.

Wakizungunza na waandishi wa habari jana ofisi za Ubalozi wa Marekani, jijini Dar es Salaam, wataalamu hao akiwamo Daktari wa Huduma za matibabu kwa raia wa Marekani wanaokuja nchini kwa ajili ya kujitolea, Dk. Arkan Ibwe, alisema kwa wenye umri wa chini ya miaka 18 mpaka sasa hakuna utafiti kuthibitisha chanjo kwao.

Alisema kwa wanaoumwa homa siku ya kuamkia kuchanjwa wanapaswa kusubiri wapone ndipo wachanje, huku wenye mzio wanatakiwa kujulikana aina ya mzio walionao ili kuangalia chanjo itakayoendana nao ili wasipate madhara.

Aidha, Daktari wa Elimu na Afya ya Jamii na Huduma za Uzazi wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Dk. Emmanuel Tluway, alisema hakuna kinachozuia wajawazito kupewa chanjo, lakini kutokana na hali zao wanashauriwa kupata ushauri kwa madaktari wao au wataalamu wa afya kabla ya kufanya uamuzi.

"Kutokana na mabadiliko ya mwili kwasababu za ujauzito wako katika uwezekano mkubwa wa kuambukizwa Uviko, ni muhimu kuangalia faida na hasara, kama faida ni kubwa basi wachanje kwa ushauri wa wataalamu wa afya, hadi sasa hakuna utafiti unaozuia wasichanje na haijaelezwa kama utafiti wa chanjo uliwahusisha wajawazito, hivyo hatuna majibu ya kisayansi kwa asilimia 100, ila wanashauriwa wachanje," alisema. Alisema wenye ugonjwa wa kifua kikuu wanapaswa kuwasiliana na madaktari wao kabla ya kufanya uamuzi, kwa kuwa wagonjwa hao huwa katika hatua tofauti.

"Wenye magonjwa ya muda mrefu kama kisukari, saratani, Ukimwi na Shinikizo la damu wanatakiwa kuchanja, lakini kubwa ni kutoa taarifa sahihi kwa mhudumu wa afya kabla ya kuchanja ili aweze kukushauri vyema," alisema Dk. Ibwe. Kuhusu kazi ya chanjo mwilini, Dk. Tluway alisema inasisimua mwili kuuwezesha kupambana kwa haraka na Uviko, inaimarisha kinga kwenye chembe hai nyeupe zinazohusika kupambana na kuangamiza, pamoja na kuangamiza vizuri vinapoingia mwilini.

Alisema chanjo nane zilizopitishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), zimepitia hatua nne za utafiti na kujiridhisha kuwa ni salama kwa binadamu yeyote huku kukiwa na madhara au maudhi madogo madogo yanayoweza kutibika kwa haraka.

Dk. Tluway aliyataja kuwa ni hatua ya kwanza ni maabara ambayo hujaribiwa kwa wanyama ili kuangalia usalama wa chanjo, hatua ya pili ni kwa binadamu wanaojitolea kushiriki ambao huwa kati ya 20 hadi 100 na kama itaonyesha madhara haitaendelea hatua nyingine.

Alisema katika hatua ya pili kinachoangaliwa ni kama chanjo ni salama, maudhi au mabadiliko yanayojitokeza, uhusiano wa chanjo na iwapo inasisimua kinga ya mwili.

Hatua ya tatu idadi ya wanaofanyiwa majaribio inaongezeka hadi kufikia 1,000 ambao huangalia ni maudhi ya muda mfupi, kinga inakaa kwa kiasi gani baada ya kuchanja na kama chanjo inakinga mwili.

Alisema kama italeta matokeo mazuri wanakwenda hatua ya tatu ambayo ni wanaofanyiwa majaribio kuwa ni kuanzia 1,000 hadi 40,000 ambao wakionyesha matokeo mazuri inapitishwa na kupewa cheti cha ithibati kama chanjo salama.

Alisema hatua ya nne ni kukusanya data za maudhi na madhara ya muda mrefu kwa waliochanjwa na linakuwa endelevu huku watu wakiendelea kupatiwa chanjo na huchukua miaka 10 au zaidi.

Naye, Daktari wa Tiba na Huduma za Sera za Afya wa Shirika la CDC, Dk. Eva Matiko, akizungumzia uwapo wa chanjo tofauti, alisema Uviko ni janga linalohitaji mapambano ya silaha tofauti na wakati mwingine zote zitumike kukabili.

Alisema Tanzania imefanyia utafiti kupitia mamlaka zake, chanjo nane zilizoorodheshwa na WHO na kujiridhisha tano ikiwamo ya Johnson and Johnson zinafaa kutumika nchini na kwamba ni salama kabisa, huku akisisitiza maudhi madogo madogo ni jambo la kawaida.

Awali, akifungua mkutano huo, Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuongoza kampeni ya kupata chanjo Julai 28, mwaka huu na kusema ni uongozi na uamuzi thabiti kwa manufaa ya wananchi wake.

"Chanjo zimekuwa sehemu muhimu za nyenzo za kulinda afya ya jamii kwa zaidi ya miaka 200 sasa. Karibu kila nchi duniani hutoa chanjo za mara kwa mara kwa watu wake ili kuwakinga dhidi ya maradhi mbalimbali," alisema. Vile vile, alisema nchini Marekani zaidi ya asilimia 99 ya vifo vipya vya Uviko-19 ni vya watu ambao hawajachanja na kwamba ukweli ni kuwa chanjo zinaweza kuokoa maisha.

# Kachero adai Sabaya alimpiga, kumsababishia maumivu diwani

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MKUU wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Wilaya ya Arusha, Mratibu Msaidizi Gwakisa Minga, amedai kwamba kipigo alichopata Bakari Msangi kutoka kwa mshtakiwa wa kwanza kilimsababishia maumivu makali.

Minga (45) alidai hayo jana alipokuwa akiendelea kutoa ushahidi wake kwa upande wa Jamhuri katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, na wenzake wawili.

Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ya unyang'anyi wa kutumia silaha ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38). Shahidi huyo pia alidai Sabaya na walinzi wake, walimpiga, kumteka nyara, kumtishia kumuuwa na kumpora Sh.390,000 wakati wakifanya uhalifu katika duka la Mohamed Saad.

Alidai kuwa Msangi wakati akihojiwa na polisi alikuwa akitokwa na damu sehemu za masikioni, ndipo walipobaini uhalifu uliofanywa na Sabaya na walinzi wenzake. Pia, alidai msangi ambaye ni shahidi wa sita katika kesi hiyo, alitambuliwa kuwa alipigwa kwa kuwa alikuwa na alama za kupigwa usoni na kwenye mashavu na alikuwa akitokwa na damu masikioni.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdalah Chavula, Minga alidai kwamba baada ya kujiridhisha kuwa amefanyiwa vitendo ambavyo ni kinyume cha sheria, alitoa taarifa kwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Arusha.

"Baada ya kutoa taarifa kwa OCD na RCO, walinipa maelezo kuwa nimjulishe aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kennan Kihongosi, kuwa watuhumiwa hawa hawakuwa na makosa baada ya kuwahoji," alidai.

Baada ya kutoa taarifa hizo kwa Kihongosi, Sabaya na Nyegu walifika tena kituoni na kuwaeleza kwamba, baada ya kuwahoji alibaini kuwa Msangi na wenzake hawakuwa na kosa lolote. "Baada ya hapo tukiwa polisi, Sabaya alimwagiza mshtakiwa wa pili kwenda kwenye gari kuchukua simu za watuhumiwa na aliwakabidhi mbele yangu. Taratibu za kukabidhiana simu zilipokamilika, Sabaya aliondoka kituoni bila ya kupekuliwa wala kukamatwa kwa kuwa alikuwa na mamlaka ya uteuzi, hivyo kiutaratibu upelelezi unapokamilika tunauwasilisha kwenye mamlaka iliyomteua," alidai.

"Pia baada ya kumaliza mahojiano nilitoa agizo vijana wale wasindikizwe hadi nyumbani kwao, kwa kuwa walikuwa na hofu sana," aliongeza kudai.

Minga aliendelea kudai kuwa baada ya tukio hilo, uchunguzi ulianza ili kuthibitisha ukweli na wakati akiendelea na majukumu yake, Februari 10, mwaka huu, saa 6:00 usiku, alipigiwa simu na OCD, akampe maelekezo ya kufika haraka kituo cha polisi kwa kuwa yupo na Msangi amepigwa na kuporwa.

"Nilipofika kituoni nilimkuta OCD. Muda si mrefu alifika Msangi akiwa ameambatana na mke wake, alikuwa na mikwaruzo na alama za kupigwa kwenye sehemu za usoni na mashavuni na alikuwa anatokwa na damu masikioni.


**TATHMINI YA ATHARI YA MRADI KWENYE MAZINGIRA**

**TANGAZO LA MRADI WA USIMAMIZI ENDELEVU WA RASILIMALI KWA AJILI YA UKUAJI WA UTALII (REGROW) KATIKA MBUGA ZA WANYAMA ZA RUAHA, UDZUNGWAN NA MIKUMI**

Serikali ya Tanzania kupitia wizara ya Maliasili na Utalii imepokea ufadhili wa mkopo wa fedha kutoka shirika la maendeleo ya kimataifa (IDA), lililoko chini ya benki ya dunia (WB) ili kugharamia utekelezaji wa mradi wa usimamizi endelevu wa rasilimali kwa ajili ya ukuaji wa utalii. Huu ni mradi wa kimkakati wenye maslahi ya kitaifa. Mbuga za wanyama Tanzania (TANAPA) chini ya wizara ya Maliasili na Utalii ni moja kati ya wakala wa utekelezaji na pia ni mnufaika mkubwa wa mradi huu.

Serikali ya Tanzania kupitia mradi huu wa kukuza utalii uliopo chini ya Wizara ya Rasilimali na Utalii, inataka kuimarisha usimamizi kwenye maeneo ya hifadhi na kukuza utalii wa asili kusini mwa Tanzania-utakaojulikana kama "Ukanda wa Kusini." Utalii huu pia utasababisha kuongezeka kwa shughuli tofauti za kujipatia kipato katika jamii zitakazochaguliwa.

Ukanda wa kusini unatoa fursa nyingi za utalii wa asili fursa ambazo kwa sasa hazitumiki sana jambo ambalo linapunguza pato la taifa kwa kiasi kikubwa sana. Kwa kuanza mradi utatoa kipaumbele katika maeneo ya hifadhi tatu ambazo ni Mbuga ya wanyama ya Mikumi (MINAPA), Ruaha (RUNAPA), na Mbuga ya wanyama ya milima ya Udzungwa (UMNP) zinazopatikana katika mikoa mitatu ya Morogoro, Iringa, na Mbeya.

Hatua ya kwanza ya kupata cheti cha mazingira kwa ajili ya mradi huu ni kufanya tathmini ya athari ya mradi kwenye mazingira na jamii (ESIA). Tathmini hii inafanywa kwa mujibu wa sheria. Sheria zinazotaka tathmini hii ifanyike in pamoja na sheria ya uhifadhi wa mazinigira ya mwaka 2004 na Kanuni za tathmini na ukaguzi wa mazingira ya mwaka 2005. Benki ya dunia pia inataka tathmini ya athari za mradi katika mazingira na jamii zifanyike, athari zinazoweza kutokea zitambuliwe na mpango wa kukabiliana na athari hizo uandaliwe ili kuondoa athari zote mbaya zinazoweza kusababishwa na mradi.

Kwa mujibu wa sheria ya usimamizi ya mazingira ya mwaka 2004 na kanuni ya tathmini na ukaguzi wa mazingira ya mwaka 2005 na marekebisho yake ya mwaka 2018, tathmini ya athari za mradi kwenye mazingira na jamii lazima iambatane na mahojiano ya wadau wa mradi katika ngazi mbalimbali na maoni ya wadau hawa yafanyiwe kazi. Pia sheria hizi zinataka tangazo la mradi litolewe kupitia vyombo ya habari ili kukusanya maoni zaidi kuhusu mradi.

Ili kupata matokeo ya tathmini ya athari za mradi kwenye mazingira na jamii, kampuni za EcoConServ. Environmental Solutions (Egypt) na MTL Consulting (Tanzania) zimepewa kazi na wizara ya Maliasili na utallii kupitia TANAPA kufanya tathmini ya athari za mradi huu kwenye mazingira na jamii (ESIA). Tathmini hii pia itaangalia athari zitakazosababishwa na ukarabati wa barabara wenye urefu wa kilometa 1,259, njia za vumbi zenye urefu wa kilometa 132.5, uwanja wa ndege, uwekaji wa miundombinu ya ujenzi kwa ajili ya wafanyakazi, vituo vya utalii pamoja na miundombinu ya maji katika mto Ruaha.

Mtu yeyote mwenye maoni, maswali au uelewa kuhusiana na athari zinazoweza kusababishwa na mradi huu kwenye mazingira na jamii awasiliane na:

**MTL Consulting Company Limited, Victoria House 9th Floor, Plot No. 37, Bagamoyo Road/Regent Estate**
**S.L.P 77894,**
**Dar es Salaam, Tanzania. Tel./Fax: +255 22 2600594**
**Cellular: +255 (0) 767 360 225**
**Barua Pepe: emasasila@mtlconsulting-tz.com**

**Mtendaji Mkuu,**
**Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC),**
**S.L.P 63154, Regent Estate, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255 22 2774889**
**Barua pepe: dg@nemc.or.tz**

216382901

## HABARI KITAIFA




Balozi wa Canada nchini Tanzania, Pamela O'Donnell na Mkurugenzi Mwakilishi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani la Umoja wa Mataifa (UN WFP) nchini, Sarah Gordon-Gibson, wakikabidhiana msaada wa Dola za Kimarekani milioni 3.74 (Sh. bil. 8.6). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Canada yatoa bil. 8.6/- kuchangia serikali mpango hifadhi ya jamii

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Canada imetoa Dola za Kimarekani milioni 3.74 (Sh. 8,654,210,000) kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani la Umoja wa Mataifa (WFP), kuchangia juhudi za kusaidia mpango wa serikali wa hifadhi ya jamii nchini.

Serikali ya Canada na WFP ni wasaidizi wakubwa wa mipango ya jamii inayotoa ulinzi dhidi ya matatizo ikiwamo kulipa fedha moja kwa moja kwa wananchi maskini.

"Serikali ya Canada inatambua umuhimu wa kuwa na mipango ya hifadhi inayolenga kuwasaidia wananchi wanaoishi katika mazingira magumu kipindi wanapopatwa na majanga," alisema Pamela O'Donnell, Balozi wa Canada nchini Tanzania.

Janga la corona linaathiri zaidi wananchi wa hali ya chini, hasa wanawake na wasichana wanaoishi maeneo ya mijini ambao tayari wanapitia changamoto za kijamii na kiuchumi.

"Afua hii inalenga kuimarisha ulinzi dhidi ya majanga na kuwafikia watu wengi zaidi wenye uhitaji, wakiwamo walioingia kwenye hali ya umaskini hivi karibuni, na kuwapatia fedha ili wakidhi mahitaji muhimu na kujenga ujasiri kwa ajili ya siku za usoni," alisema.

Taarifa iliyotolewa na WFP jana kwa vyombo vya habari ilisema mchango wa Serikali ya Canada unaonyesha kujitoa kwao katika kusimama pamoja na washirika wao wa kitaifa na wadau wa maendeleo kushughulikia janga hilo la kimataifa ambalo sio la kawaida.

Nchini Tanzania, WFP inafanya kazi na serikali kusaidia mfumo wa kijamii unaotoa ulinzi dhidi ya matatizo kupitia utoaji wa fedha kwa walengwa moja kwa moja na kazi za umma, unaosimamiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (TASAF), kuzifikia kaya maskini.

"Kwa mchango huu kutoka Serikali ya Canada, WFP itaweza kuimarisha msaada huu kwa manufaa ya watu wanaoishi katika hali ya umaskini maeneo ya mijini. Mkazo utawekwa katika kushughulikia umaskini unaotokana na jinsia, ukiwamo ambao unakabili kaya zinazoongozwa na wanawake."

"Tunashukuru sana Serikali ya Canada kwa mchango walioutoa kwa WFP kwa lengo la kusaidia mpango wa kitaifa wa hifadhi ya jamii. Mipango ya kijamii inayotoa ulinzi dhidi ya matatizo ni muhimu katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula na lishe na kubadilisha maisha ya wananchi maskini, hususan wanawake, ambao wana jukumu la kuhakikisha uhakika wa chakula na lishe ndani ya kaya," alisisitiza.

Mkurugenzi huyo alisema Serikali ya Canada inaonyesha inavyojitoa kujenga ujasiri wa Watanzania maskini.

Nchini Tanzania, WFP inafanya kazi kuboresha maisha ya familia maskini kwa kupambana na utapiamlo, kusaidia wakulima wadogo, kutoa msaada wa chakula kwa wakimbizi na kutumia ufumbuzi bunifu kwa ajili ya kupata matokeo halisi.

"Sisi ni shirika la kibinadamu kubwa zaidi duniani, tunaokoa maisha wakati wa maafa na kutumia utoaji wa msaada wa chakula kama njia ya kuleta amani, utulivu na ustawi kwa watu walioathirika na migogoro, maafa na madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi," alisema.


The Guardian Limited

**VACANCY**

**Freelancer Sales Executive**

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.**

216387602


# Majaji watatu kusikiliza kesi kikatiba ya Mbowe korti kuu

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya kikatiba iliyofunguliwa Mahakama Kuu na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akilalamikia ukiukwaji wa haki za kikatiba katika kesi ya ugaidi, imepangwa kusikilizwa na jopo la majaji watatu Jumatatu ijayo.

Kesi hiyo imepangwa jana kusikilizwa na majaji John Mgeta, Steven Magoiga na Leila Mgonya.

Wakili wa Mbowe, Peter Kibatala, alidai kesi hiyo inatarajia kutajwa kwa mara ya kwanza mbele ya jopo hilo siku hiyo saa 8:00 mchana.

Agosti 2, mwaka huu, Mbowe kupitia Kibatala aliwasilisha maombi Mahakama Kuu akitaka itamke kwamba kuna ukiukwaji wa haki za kikatiba dhidi ya mteja wake katika kesi ya ugaidi inayomkabili.

Mbowe alifungua maombi dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini na Mwanasheria Mkuu wa Serikali akidai wamevunja haki zake kikatiba kwa kushindwa kumpa nafasi ya kusikilizwa kikamilifu.

Katika maombi yake, analalamikia kuvunjwa kwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Uhujumu Uchumi ambayo ameshtakiwa nayo kwa tuhuma za ugaidi. Wakili Kibatala anadai kwa mujibu wa sheria hizo, mtuhumiwa anataka asishikiliwe zaidi ya saa 48 kituo cha polisi na akifikishwa mahakamani hakimu anatakiwa kuhakikisha ameyaelewa mashtaka yanayomkabili.

Anadai Mbowe alishikiliwa Kituo cha Polisi Oysterbay, Dare s Salaam tangu Julai 21 hadi Julai 26, mwaka huu, alipofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kushtakiwa kwa ugaidi.

Katika maombi hayo anadai sheria zimevunjwa, mteja wake alikaa kituoni zaidi ya saa 48, alilazwa sakafuni bila kujali usalama wa afya yake, hivyo wamevunja haki zake za kikatiba, wamemtesa na kumdhalilisha.

Polisi wanadaiwa kuvunja haki hizo kwa kushindwa kumpa nafasi ya kumsikiliza kikamilifu na kwamba walishindwa kutoa taarifa kwa mawakili wake ama ndugu yake wa karibu.

Kibatala pia anadai kuwa Mbowe alipelekwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, bila kuambiwa anakwenda wapi na alipopanda kizimbani, mahakama ilikiuka haki za kikatiba kwa kushindwa kumuuliza kama ameelewa mashtaka yanayomkabili.

"Alitakiwa afahamishwe mashtaka yake kiufasaha, mashtaka mazito, mahakama haijamuuliza kaelewa au la zaidi ya kumwambia mahakama haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo," alidai Kibatala katika maombi yake.

Pia anadai Mbowe hakupewa hati ya mashtaka hadi Julai 27 mawakili wake walipokwenda naye gerezani.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tukio la mlipuko TANESCO liwe fundisho kwa watu wote

**MAPEMA** wiki hii kituo cha kupokea na kupooza umeme cha Msamvu mkoani Morogoro kililipuka na kusababisha taharuki kwa wananchi wanaokaa na kufanya shughuli zao katika eneo hilo.

Licha ya kuzua taharuki kwa wananchi, pia lilisababisha sehemu kubwa ya nchi kukumbwa na ukosefu wa umeme, hivyo kuathiri shughuli mbalimbali za uzalishaji na huduma muhimu kama afya na elimu. Tukio hilo lilisababisha umeme kukatika mara kwa mara na kutishia kusababisha maafa kama ya kuharibika kwa mali zinazotumia umeme.

Tukio la namna hiyo ni la pili kwa eneo hilo na limetokea watu wakiwa bado na mawazo kutokana na mlipuko wa lori la mafuta uliosababisha watu kadhaa kupoteza maisha yao.

Hata hivyo, wataalamu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) walifanya kazi ya ziada kufanya matengenezo katika maeneo mengine ili kuhakikisha wananchi hawapati shida ya umeme na hatimaye kuathiri shughuli zao za kila siku.

Kutokana na janga hilo, serikali imeunda kamati maalum ya uchunguzi juu ya chanzo cha tukio hilo. Kamati hiyo kupitia hadidu za rejea ilizopewa, inatarajiwa kukamilisha kazi yake ya kuwasilisha ripoti ndani ya siku chache zijazo.

Yako matukio mbalimbali ambayo yameligharimu taifa kwa maana ya uharibifu wa miundombinu, watu kupoteza mali zao na hata wengine kupoteza maisha. Pamoja na kuwapo kwa matukio kama hayo, bado vyombo husika havijachukua hatua za kudhibiti au kukinga majanga kabla ya kutokea na kusababisha athari kubwa.


Miongoni mwa matukio hayo ni kuzama kwa vyombo vya usafiri wa majini katika Bahari ya Hindi na Ziwa Victoria, ajali za barabarani, milipuko ya magari yenye vimiminika hatarishi kama mafuta na ajali za treni na ndege katika baadhi ya maeneo. Matukio hayo kwa kiasi kikubwa yamesababisha watu kupoteza maisha na vyombo vyenyewe kuharibika.

Tukio la Morogoro, kwa mfano, limesababbabisha hasara kubwa si kwa TANESCO tu bali kwa serikali kutokana na kuteketea kabisa. Hatua hiyo itaifanya serikali kutafuta fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa kituo chenye hadhi kama hiyo ili kuhakikisha umeme unapatikana bila matatizo.

Kwa sehemu kubwa, matukio hayo yamkini yamekuwa makubwa na matokeo yake kuwapo kwa hasara kubwa. Sababu hasa za kuwapo kwa majanga kama hayo ni utayari hafifu wa vyombo vya udhibiti hasa katika eneo la ukaguzi na kuweka tahadhari dhidi ya majanga mbalimbali.

Matukio hayo husussan lile la Morogoro, linapaswa kuwa fundisho kwa taasisi na watu mbalimbali waliopewa wajibu wa kuratibu, kusimamia na kuratibu sekta mbalimbali ili kuwalinda Watanzania na mali zao. Mamlaka hizo na wahusika wanapaswa kuchukua tahadhari mbalimbali ili kuhakikisha majanga kama hayo hayajitokezi mara kwa mara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Mary Geofrey

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kunyonyesha kuwe kama kula 'ni lazima'

**UNYONYESHAJI** wa maziwa ya mama kwa miezi sita mfululizo ni msingi wa maisha, afya, lishe bora na uhakika wa chakula kwa mtoto katika hali ya kawaida na kunapotokea mabadiliko ya dharura kiafya.

Maziwa ya mama ni miongoni mwa haki za msingi za binadamu ambayo inapaswa kuheshimiwa, kulindwa na kutekelezwa kikamilifu.

Kuwatenganisha mama na mtoto, huathiri kuanza utaratibu na mtiririko wa unyonyeshaji ndani ya saa moja baada ya mama kujifungua na huathiri mfumo wa unyonyeshaji katika miezi sita ya mwanzo na kuendelea.

Maambukizi ya virusi vya COVID-19 yameathiri upatikanaji wa huduma ya unyonyeshaji watoto maziwa ya mama ni kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC).

Zinathibitisha kuwa hakuna uhusiano kati ya unyonyeshaji maziwa kutoka kwa mama na madhara kwa mtoto au kumwambukiza virusi vya corona.

"Maziwa ya mama mwenye ugonjwa huo ni salama kwa mtoto wake, anashauriwa kuendelea kunyonyesha kwa kuzingatia tahadhari za kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji safi tiririka na sabuni na kukaa karantini wakati akiendelea kunyonyesha," anasema Dk. Ester Nkuba kutoka TFNC.

Kwa mwaka huu, kauli mbiu ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani ni 'kulinda unyonyeshaji wa maziwa ya mama ni jukumu letu sote'.

Kauli mbiu hii inabeba ujumbe unaoonyesha umuhimu wa uwajibikaji wa pamoja wa wadau wote katika ngazi zote ili kutetea, kulinda na kuendeleza taratibu sahihi za unyonyeshaji watoto maziwa ya mama.

Kauli mbiu hiyo pia inajenga mazingira wezeshi kwa wanawake kuwanyonyesha watoto wao kwa ufanisi.

Malengo ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani kwa mwaka huu ni kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda unyonyeshaji.

Kadhalika ni kuhimiza jukumu la jamii la kulinda, kutetea na kuendeleza unyonyeshaji ili kulinda afya ya mama na mtoto na ushirikiano wa wadau ikiwamo sekta binafsi na asasi za kiraia ili kuleta matokeo chanya.

Malengo mengine ni kuhamasisha jamii ichukue hatua za kulinda unyonyeshaji ili kuboresha afya ya umma.

Mama anayenyonyesha anatakiwa kuwa na lishe bora kutokana na kuwa na mahitaji makubwa ya virutubishi mwilini kwa ajili ya afya yake na kwa ajili ya kutengeneza maziwa ya mtoto.

Kwa sababu hiyo, ni muhimu mama anayenyonyesha kula milo kamili zaidi ya mitatu kwa siku na kula kitu kingine kati ya mlo na mlo.

Umuhimu wa ulaji unaofaa kwa mama anayenyonyesha ni kuwa na afya bora kwa sababu humpatia virutubishi vya kutosha kutokana na ongezeko la mahitaji ya virutubishi wakati wa unyonyeshaji

Kadhalika huwezesha mwili wa mama kutengeneza na kutoa maziwa ya kutosha kadri mtoto anavyohitaji.

Lishe bora huimarisha kingamwili za mama zidi ya maradhi mbalimbali na kuzuia upungufu wa damu kwa mama na mtoto, huongeza akiba ya madini chuma ambayo hutumika kwa mama na kwa mtoto kupitia maziwa ya mama.

Aidha, husaidia kumuwezesha mtoto kuwa na afya bora kutokana na kupata maziwa ya kutosha kutoka kwa mama.

Kwa mama anayenyonyesha anatakiwa kuzingatia kula milo kamili zaidi ya mitatu kwa siku, mlo kamili ni mlo wenye chakula mchanganyiko angalau chakula kimoja kutoka katika kila kundi la chakula.

Mama anatakiwa pia kumeza vidonge vya kuongeza damu (FEFO) kwa kipindi cha miezi mitatu baada ya kujifungua na kutumia vyakula vilivyoongezwa virutubishi, kama vile unga wa ngano, unga wa mahindi, mafuta ya kupikia na kutumia chumvi yenye madini joto.

Kuongeza ulaji wa vyakula vyenye asili ya wanyama mfano nyama, kuku, mayai, maziwa, samaki, dagaa vina virutubishi vya aina mbalimbali kwa wingi ikiwamo madini chuma ambayo husaidia kuongeza damu mwilini.

Mama anayenyonyesha pia ni muhimu kusaidiwa kazi nzito ili apate muda wa kutosha wa kupumzika na kumnyonyesha mtoto mara kwa mara kila anapohitaji, usiku na mchana.

Kupitia maadhimisho haya jamii inapata jukwaa la kukumbushana kuhusu umuhimu wa maziwa ya mama na jinsi yanavyosaidia kuboresha afya ya watoto wachanga.

HABARI KITAIFA

# Walichoteta upinzani, Waziri wa Marekani

**Na Romana Mallya**



VIONGOZI wa vyama vya upinzani wamekutana na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Balozi Victoria Nuland, kubwa likiwa ni suala la demokrasia nchini.

Akizungumza na Nipashe jana, Naibu Katibu Mambo ya Nje wa Chama cha ACT-Wazalendo, Bonifasia Mapunda, alisema mazungumzo yao na kiongozi huyo, yalihusisha vyama vinne vya upinzani.

"ACT-Wazalendo tuliwakilishwa na Kiongozi wetu, Zitto Kabwe (pichani), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika (Katibu Mkuu), Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba (Mwenyekiti) na NCCR Mageuzi," alisema.

Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo alisema katika kikao hicho, moja ya ajenda zao ilikuwa kujadiliana kuhusu hali ya demokrasia nchini.

"Naibu Waziri alitoa salamu za Rais Samia Suluhu Hassan, kwa vyama vya siasa kwamba ana nia ya kufanya mazungumzo na viongozi wa vyama vya siasa, viongozi walipokea kwa mtazamo chanya," alisema.

Alibainisha kuwa mjadala mkubwa ulilenga kuona haja ya kuwa na majadiliano ya kisiasa hususani kujadili hali ya demokrasia nchini na viongozi wa vyama hivyo vya upinzani walimweleza naibu waziri matatizo ambayo wanapitia kwa sasa.

"Mfano, unapozungumzia demokrasia maana yake ni mfumo ambao upo kisheria ambapo watu wanatakiwa kuishi kwa kuufuata, walieleza demokrasia yetu kutokuwa na haki.

"Kumekuwa na kuonewa kwa viongozi wa upinzani, mikutano ya hadhara kuzuia ambayo ipo kisheria, wananchi kutoshiriki katika siasa na uchaguzi," alisema.

Alisema mapendekezo mawili makubwa ya viongozi hao wa upinzani kwa kiongozi huyo wa Marekani, ni kuitaka Serikali ya Marekani kutumia uwezo wake wa kidiplomasia kuishawishi Tanzania kurejea katika misingi ya kidemokrasia na utawala bora.

Pia, waliomba Marekani kufanya kazi kwa karibu na vyombo ambavyo vipo ndani ya nchi vinavyohusiana na demokarasia, ili kuendelea kupata taarifa na mijadala ya masuala ya demokrasia.

# Bodi yasikitishwa tukio la moto TANESCO

**Na Frank Kaundula**, MOROGORO

BODI ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) imetembelea eneo lililoathiriwa na mlipuko wa umeme maeneo ya Tungi na kueleza kusikitishwa na uharibifu ambao umesababisha taifa kupata hasara.

Wajumbe wa bodi hiyo walitembelea eneo hilo juzi jioni na kujionea chanzo cha mlipuko huo ikiwa ni pamoja na baadhi ya mitambo ya umeme katika kituo cha kupokea na kupooza umeme cha Msamvu ilivyoathiriwa.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Alexander Kyaruzi, alisema wamesikitishwa na tukio hilo lililotokea juzi asubuhi na kuzua taharuki kubwa kwa wananchi wa Morogoro hasa wale wanaoishi maeneo ya jirani zaidi.

"Tumesikitishwa na kitendo hiki kwani mbali na tarahuki kwa wananchi pia wananchi wa mkoa huu wa Morogoro na mkoa ya jirani walijikuta kwenye wakati mgumu ya kukosa huduma muhimu ya umeme," alisema.

Dk. Kyaruzi alisema kitendo cha kukosa huduma ya umeme ni hasara kubwa kwa taifa kwa kuwa shughuli zote za uzalishaji zinazotegemea nishati hiyo, hivyo kuagiza ufumbuzi wa haraka uchukuliwe.

"Tunaona kuwa huduma ya umeme imerudi, lakini tunatambua fika kuwa yapo baadhi ya maeneo kutokana na hitilafu hii. Bado huduma hii haijarudi, hivyo natoa wito wangu kwa wataalamu wa TANESCO kulifanyia kazi hilo," alisema.

Hata hivyo, alipongeza hatua zilizochukuliwa na uongozi wa mkoa wa Morogoro na kutaka hatua sitahiki kuchukuliwa kwa wote watakaobainika kusababisha moto huo.

Pia aliwashukuru TANESCO mkoa kwa kufanya jitihada kubwa zilizowezesha kupatikana kwa huduma ya umeme. Aliagiza wataalamu kuhakikisha maeneo ambayo bado yana changamoto hiyo kuitatua haraka.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, aliipongeza TANESCO kwa kitendo chake cha kurudisha umeme ndani ya muda mfupi baada ya tukio la moto huo na kusisitiza kwamba hatarajii kuona tukio hilo likijirudia.

Shigela alisema mbali na kuunda tume kwa ajili ya uchunguzi wa tukio hilo ili hatua zichukuliwe, aliitaka TANESCO kuhakikisha inaweka vizuri miundombinu yake ili kusitokee tatizo linaloweza kuathiri upatikanaji wa umeme mkoani hapa.


TOL Gases Limited
We Deliver

**TOLGASES LIMITED**
**EXTRACT STATEMENTS FOR THE YEAR ENDED ON 31 DECEMBER 2020**

**EXTRACT OF THE STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2020**

| | 2020 TZS '000 | 2019 TZS '000 |
|---|---|---|
| Revenue | 19,816,325 | 17,252,567 |
| Cost of sales | (11,372,996) | (9,503,163) |
| **Gross profit** | **8,443,329** | **7,749,404** |
| Other income | 77,593 | 125,407 |
| Operating expenses | (3,797,948) | (3,735,887) |
| Trade receivables impairment release | 30,997 | 77,904 |
| **Operating profit** | **4,753,971** | **4,216,828** |
| Finance costs | (916,032) | (1,130,167) |
| **Profit before tax** | **3,837,939** | **3,086,661** |
| Income tax expense | (1,493,808) | (832,690) |
| **Profit for the year** | **2,344,131** | **2,253,971** |
| Other comprehensive income | - | - |
| **Total comprehensive income** | **2,344,131** | **2,253,971** |
| Earnings per shares (TZS) | | |
| – Basic | 0.04076 | 0.0392 |
| – Diluted | 0.04076 | 0.0392 |

**EXTRACT OF STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2020**

| | 2020 TZS '000 | Restated 2019 TZS '000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| **Non-current Assets** | | |
| Property, plant and equipment | 25,391,918 | 20,601,936 |
| Right-of-use assets | 325,331 | 49,876 |
| Intangible asset | 370,875 | 153,576 |
| | **26,088,124** | **20,805,388** |
| **Current assets** | | |
| Inventories | 4,548,373 | 5,296,263 |
| Trade and other receivables | 5,818,230 | 4,524,264 |
| Cash and bank balances | 604,357 | 374,537 |
| | **10,970,960** | **10,195,064** |
| Asset held for sale | 2,674,275 | 2,658,558 |
| **TOTAL ASSETS** | **39,733,359** | **33,659,010** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | |
| **Equity** | | |
| Share capital | 5,750,596 | 5,756,030 |
| Share premium | 6,762,049 | 6,756,615 |
| Retained Earnings | 10,462,810 | 9,117,558 |
| | **22,975,455** | **21,630,203** |
| **Non-current liabilities** | | |
| Long term borrowings | 3,806,949 | 3,747,465 |
| Lease liabilities | 45,486 | 39,751 |
| Deferred tax liability | 2,257,024 | 1,722,551 |
| | **6,109,459** | **5,509,767** |
| **Current liabilities** | | |
| Trade and other payables | 1,869,927 | 1,109,951 |
| Lease liabilities | 189 | 6,016 |
| Tax payable | 867,563 | 521,700 |
| Bank overdraft | 3,014,454 | 3,176,570 |
| Cylinder deposits | 459,052 | 658,281 |
| Current portion of loans | 4,437,260 | 1,046,522 |
| | **10,648,445** | **6,519,040** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **39,733,359** | **33,659,010** |

# Wanawake wapewa nguvu kumiliki ardhi

**Na Frank Monyo**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Legal Services Facility (LSF) kwa kushirikiana na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo, limezindua mradi utakaowawezesha wanawake wanaomiliki vipande vya ardhi katika wilaya hiyo kupata hati za umiliki wa ardhi zitakazowawezesha kujikwamua kiuchumi na kupata elimu juu ya masuala ya ardhi.

Akizungumza Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema mradi huo ujulikanao 'Hati Yangu Maisha Yangu', umeanzishwa mahususi ili kukabiliana na vikwazo vinavyowakumba wanawake wa hali ya chini wanaomiliki ardhi ambao wameshindwa kukamilisha umilikishwaji kutokana na kutomudu gharama zitokanazo na upatikanaji wa hati.

"Tunayo furaha kubwa kubuni mradi huu na kutoa ruzuku kwa TAWLA kuutekeleza kwa lengo la kuboresha maisha ya wanawake na kusaidia kupunguza umaskini.

"LSF tunatambua wanawake wanapitia changamoto nyingi sana zikiwamo unyanyasaji wa kijinsia, kutopata fursa sawa katika masuala ya kiuchumi, kiuongozi lakini wamekuwa na majukumu mazito katika kulea na kuhakikisha ustawi wa familia zao.

"Hivyo, tunaamini kupitia mradi huu tutawawezesha kumiliki ardhi walizonazo na kuzitumia katika kupata mitaji na kukuza shughuli zao za kiuchumi kwa manufaa ya familia zao na taifa kwa ujumla," alisema Ng'wanakilala.

Alisema mradi huo pia umelenga kutoa elimu kwa wananchi juu ya sheria za ardhi, umilikishwaji ardhi, haki ya kurithi na kumiliki ardhi ili kuongeza uelewa na kupunguza matatizo yanayowaathiri wanawake kwenye sekta hiyo.

Aliongeza kuwa kupitia mradi huo, wanatarajia kuwafikia wanawake takribani 2,000 kwa kuwapatia elimu na zaidi ya wanawake 300 watapata hati miliki zao kwa kuchangia gharama kidogo. "LSF imejipanga kuchangia gharama za urasimishaji na upatikanaji wa hati kwa asilimia 80 na mwananchi atatakiwa kuchangia asilimia 20 tu.

"Hii ni nafasi ya kipekee kwa wanawake wanaoishi katika Wilaya ya Ubungo kunufaika kwa kuchangamkia fursa hii," alisisitiza Ng'wanakilala.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ubongo, Beatrice Kwai, aliishukuru TAWLA kwa utekelezaji wa programu pamoja na LSF ambao ni wafadhili kwa kuweza kutambua vikwazo vinavyowakabili wanawake katika jamii na kuamua kuchagua kutekeleza mradi hupo katika Halmashauri ya Ubungo.

"Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo Mpango wa Kitaifa wa Kudhibiti na Kuzuia Makazi Yasiyopangwa (2012-2021) katika maeneo ya miji na mijini.

"Dar es Salaam ni moja ya mikoa inayonufaika na mpango huo hususani katika Wilaya ya Ubungo.

"Zoezi hili linalenga katika kupanga maeneo ya miji na mijini ili kuchochea maendeleo pamoja na kuwapo na ulinzi kwa wamiliki wa vipande vya ardhi ili kupunguza migogoro ya ardhi ambayo imekuwa mingi mno," alisema. Aliongeza kuwa uendelezaji wa makazi katika Wilaya ya Ubungo umeendelea kuimarika kwa kutekeleza programu na mikakati ya upangaji na urasimishaji makazi.

"Ni matumaini yetu kupitia programu ya 'Hati Yangu Maisha Yangu', itasaidia kuwawezesha wanawake hususani wasiojiweza katika Kata za Mbezi, Msigani, Kwembe, Goba na Kibamba kupimiwa maeneo yao kwa kuchangia gharama za upimaji.

"Vilevile tunaamaini kupitia elimu itakayotolewa kwa jamii itasaidia kubadilisha dhana potofu juu ya haki za wanawake katika kumiliki ardhi pamoja na kuongeza uelewa kwa wanawake katika masuala ya umiliki wa ardhi na jinsi ya kutumia ardhi kama vyanzo vya uchumi," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TAWLA, Tike Mwambipile, alisema: "TAWLA chini ya ufadhili wa LSF, kwa kuthamini mchakato wa urasimishaji wa ardhi unaoendelea hivi sasa nchini na ulinzi wa haki za wanawake katika kumiliki ardhi, itafanya kazi kwa karibu sana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo ili kufanikisha wanawake pamoja na makundi maalum kupimiwa ardhi na kupatiwa hati miliki."

## TBS yaokoa bil. 2.7/- ukaguzi wa magari

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imeokoa Sh. bilioni 2.7 tangu ilipoanza kufanya ukaguzi wa magari ndani ya nchi mwaka huu fedha ambazo kwa utaratibu wa awali wangelipwa mawakala waliokuwa wakifanyakazi hiyo nje ya nchi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo, alipofanya ziara katika vituo viwili vya ukaguzi wa magari yanayotoka nje, kimoja kikiwa bandarini na kingine cha UDA.

Profesa Mkumbo, alisema utaratibu huo umekuwa wa manufaa makubwa kwa serikali kwa kuwa kuanzia Aprili hadi Agosti mwaka huu, TBS kwa niaba ya serikali wamekusanya takribani Sh. bilioni 3.9, kwenye fedha hiyo kama wangeendelea na utaratibu wa zamani shirika kwa niaba ya serikali lingepata asilimia 30 na asilimia 70 (sawa na sh. bilioni 2.7) zingebaki kwa mawakala waliokuwa wakifanyakazi kazi hiyo.

Alisema serikali kwa kuamua kutekeleza mpango huo inaokoa fedha nyingi ambazo zilikuwa zikibaki nje ya nchi kwa kuwa kwa kipindi cha takribani miezi mitatu pekee imekusanya Sh. bilioni 3.9 na fedha hiyo inaingia Mfuko Mkuu wa Serikali.

Alisema utaratibu huo mpya unakwenda vizuri na wanafurahishwa na TBS ilivyojipanga vizuri kutekeleza jukumu hilo.

"Nafurahi utaratibu huu unazidi kuimarika ambapo taarifa ambayo nimeipata hadi kufikia Agosti 3, yalikaguliwa magari 11,179 na kati ya hayo 7,707 yalikidhi ubora na mengine ambayo yalibaki yalienda kutengenezwa kwenye gereji zetu zinazomilikiwa na Watanzania," alisema.

Alisema jambo la pili kupitia mpango huo vijana wengi wameajiriwa kwa ajili ya kufanyakazi ya ukaguzi wa magari hayo, lakini pia na kwenye gereji kunachangamka kwa kuwa wanapata kazi za kufanya.

"Kwahiyo niwaombe Watanzania waendelee kuunga mkono shughuli hii. Lakini natoa wito kwa wananchi wanaoagiza magari na wafanyabiashara wanaofanyakazi ya kuondoa mizigo bandarini kwamba utaratibu huu ni mzuri, waendelee kutoa ushirikiano pale ambapo kuna upungufu watueleze kama ambavyo wamekuwa wakifanya na sisi kupitia TBS tunafanya marekebisho, tunaamini kwamba baada ya muda mambo yataboreshwa vizuri zaidi," alisema.

Meneja wa Ukaguzi wa Bidhaa Zinazotoka Nje wa TBS, Saidi Mkwawa, alisema kwa mapato hayo ya Sh. bilioni 3.9 ambayo yametokana na ukaguzi huo, kama ukaguzi ungekuwa unafanyika nje ya nchi, serikali ingepata asilimia 30 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 1.3.

Alisema kwa mapato hayo serikali imeokoa Sh. bilioni 2.7 zilizokuwa zinabaki nje na inaonyesha ni kwa kiasi gani TBS inatekeleza maelekezo ambayo imepewa na Serikali ya Awamu ya Sita, ambayo inasisitiza kuboresha biashara na kukusanya mapato.



Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, akipatiwa chanjo ya ugonjwa wa Corona, katika kituo cha Afya cha Sabasaba, Manispaa ya Morogoro, jana. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

## Mbunge ataka wapotoshaji kuhusu chanjo wapuuzwe

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, amewataka wananchi wa jimbo hilo kuwapuuza wanaotoa kauli potofu kuhusu chanjo ya corona huku akiwasisitiza kujitokeza kwa ajili ya kupatiwa huduma hiyo.

Abood alisema hayo jana baada ya kupatiwa chanjo katika Kituo cha Afya cha Sabasaba, mjini hapa.

Alisema kumekuwapo na maneno mengi hasa kwenye mitandao kuhusu chanjo hiyo kitu ambacho alisema si cha kweli kwa kuwa serikali haiwezi kufanya jambo baya kwa wananchi wake, hivyo kutaka watu wa aina hiyo wapuuzwe na wasipewe nafasi.

"Yako maneno mengi katika mitandao na sehemu zingine ya vitisho kuhusu chanjo hii ya corona. Nawahakikishia ni salama na mimi mbunge wenu nimechanjwa. Naomba tuiamini serikali katika hili," alisema.

Mbunge huyo aliwataka wananchi ndani ya Manispaa ya Morogoro na maeneo mengine walio tayari na walioko katika makundi yaliyotajwa kwa ajili ya kupewa kipaumbele kupata chanjo hiyo, kujitokeza katika vituo vilivyotengwa kwa huduma hiyo.

Nao baadhi ya wananchi waliojitokeza kupata chanjo hiyo walisema kwa nyakati tofauti kuwa serikali inapaswa kupongezwa kwa kuwa hatua hiyo imesaidia kupunguza maambukizi na kusambaa kwa ugonjwa huo.

Walisema sababu zilizowafanya wakubali kupata chanjo hiyo ni kutokana na watu wengi kuishi kwa hofu, vilipoingia hapa nchini wengi wamekuwa wakiishi kwa hofu na kuogopa hata kwenda tangu ugonjwa huo ulipoingia.

Mkazi wa Kilakala Manispaa ya Morogoro, Ashura Athumani alisema tangu virusi vya corona vilipoingia nchini amekuwa akiishi kwa hofu hasa hili wimbi la tatu limekuwa linamwongopesha hata kukaribisha wageni nyumbani mwake.

Alisema baada ya kupata taarifa ya ujio wa chanjo mkoani Morogoro, alijiandaa kisaikolojia na kukubali kuchanjwa kwa ajili ya kijikinga na corona na kwamba anajitahidi kuwa balozi mzuri wa kutoa elimu zaidi.

# Makamba aahidi umeme vijiji vyote

**Na Thobias Mwanakatwe,** LUSHOTO

MBUNGE wa Bumbuli, January Makamba, amesema atahakikisha vijiji na vitongoji katika jimbo hilo ambavyo havijapata umeme, vinafikiwa na huduma hiyo ili kusukuma gurudumu la maendeleo na kuondokna na adha ya kukosa nishati hiyo.

Akizungumza katika ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo jana, Makamba alisema wakati anaingia madarakani alikuta kata nne tu ndizo zilikuwa na huduma ya umeme lakini hivi sasa kata 15 kati ya 18 katika jimbo hilo zimeshafikiwa.

Makamba alizitaja kata ambazo hazina umeme kuwa ni Milingano, Kwemkomole na Kisiwani.

Mbunge huyo alisema alipoingia madarakani aliahidi kupeleka umeme kila kijiji na ahadi hiyo ameitimiza kwa kiasi kikubwa na sasa anapigania kata zilizobaki zipate awamu nyingine na baadaye vitongoji vyote.

"Kama umeme huu ungekuwa haujafikika kabisa halafu mbunge akaahidi kupeleka kwenye vitongoji basi ujue huyo ni tapeli. Naomba mwendelee kusubiri umeme utafika kwani maendeleo yakipatikana hata mimi mbunge nafurahi," alisema.

Makamba alisisitiza kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inaelekeza kuwa maeneo yote ambayo hayajafikiwa na umeme yafikiwe ili wananchi wa maeneo husika waondokane na giza. Alisema dalili ya kwamba umeme utafika maeneo yote zinaonekana kwa kuwa baadhi ya nguzo zinaoneka tofauti na miaka ya nyuma iliyopita hakukuwa na nguzo hata moja.

Mbali na umeme, Makamba aliahidi uboreshaji wa miundombinu mingine zikiwamo shule za msingi na sekondari katika awamu hii lengo likiwa ni kuweka mazingira bora ya kujifunzia wanafunzi ili kuwapa hamasa ya kuongeza ufaulu wao katika masomo yao.

Alisema kwenye elimu kuna changamoto kubwa sana na kila shule inaupungufu wa vitu mbalimbali na kwamba hili ni tatizo la nchi nzima na changamoto hiyo inasababisha ufaulu duni.

Baadhi ya wananchi wa jimbo hilo walimpongeza mbunge huyo kwa kuendelea kuwasaidia katika suala la maendeleo, hivyo wanaamini kwa kushirikina na serikali umeme utafika kila mahali na ahadi alizotoa za kumaliza changamoto zinakamilika.




Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Esther Mahawe (kushoto), akikabidhi zawadi ya zaidi ya Sh. milioni 179 kwa mshindi wa zawadi kubwa ya promosheni ya Vodacom Tusua Mapene, Ramadhani Bwaniki katika hafla iliyofanyika Uwanja wa Katubuka, mjini Kigoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafurahia DED kuteuliwa tena

**Na Steven William,** MUHEZA

BAADHI ya wananchi wa Muheza mkoani Tanga, wamefurahia kubaki kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Nassib Mmbaga, kutokana na uteuzi uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi hao walisema hatua hiyo huenda imetokana na utendaji wake mzuri wa kazi hasa kusimamia miradi ya maendeleo, kusimamia matumizi ya fedha za serikali na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kufikia asilimia 94.

Juma Hassan, mkazi wa mji wa Muheza, alisema mkurugenzi huyo amebaki bila kuhamishwa wala kuachwa kwa kuwa amekuwa akijitahidi katika utendaji mzuri wa kazi za kusimamia miradi ya maendeleo ikiwamo ukusanyaji mapato ya ndani.

Sambamba na hilo, alisema amesimamia matumizi fedha za serikali katika

miradi mbalimbali ya maendeleo hasa zile zilizoletwa kutoka Serikali Kuu.

"Amekuwa akijitahidi kutoa fedha za mapato ya ndani za asilimia 10 kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya vijana, wanawake na wenye ulemavu," alisema.

Naye Hidaya Selemani, mkazi wa Majengo Muheza Mjini, alisema

wananchi wengi wamefurahia mkurugenzi huyo kubaki Muheza kwa kuwa amefanya mambo mazuri ya maendeleo.

Alisema mkurugenzi huyo amekuwa akisikiliza kero na shida za watu na

kuzipatia ufumbuzi katika ofisi yake ikiwa pamoja na watumishi wake na wananchi wa kawaida.

Rajabu Athuman, mkazi wa kijiji cha Lusanga, alisema toka mkurugenzi huyo afike Muheza, wilaya imepiga hatua katika sekta mbalimbali na kuongeza kuwa wana imani kubaki kwake kutaongeza chachu ya wilaya kupiga hatua zaidi kimaendeleo.

Kwa upande wake, Mmbaga alipozungumza na gazeti hili, alisema anamshukuru Mungu kwa kuteuliwa tena na Rais kuendelea na cheo hicho na pia kubaki katika kituo hicho cha kazi huku akiahidi kuchapa kazi zaidi kwa maendeleo ya wilaya.

# Asasi yapania kuwainua wakulima wa parachichi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

UMOJA wa Wakulima wa Maparachichi na Kilimo Hai kupitia Asasi ya Njombe Southern Highland Development Association (NSHIDA), wamedhamiria kupanua wigo wa uzalishaji wa zao hilo kwa kuwataka wawekezaji kufika kuwekeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa NSHIDA, Frank Msigwa, alisema mpango huo unalenga kupokea wawekezaji mbalimbali wenye nia ya kuwekeza katika kilimo cha maparachichi na makademia.

Kupitia asasi hiyo, wawekezaji watakuwa chini ya usimamizi kuanzia upatikanaji wa mashamba na usimamizi hadi msimu wa mavuno. Lengo ni kuongeza uzalishaji maradufu zaidi ya sasa kutokana na uhitaji mkubwa wa maparachichi katika soko la dunia.

Msigwa alisema hatua hiyo imechukuliwa kutokana na wakulima wengi kukosa utaalamu wa kilimo licha ya kuwa na nia ya kuwekeza. Alisema asasi hiyo imelazimika kuzindua mfumo wa kusimamia mashamba ya wakulima kuanzia hatua ya awali hadi mavuno kwa gharama ndogo.

"Kutokana na uhitaji mkubwa wa maparachichi na makademia duniani, tumeona tuanzishe hii programu ili kuwasaidia Watanzania wenzetu na wasio Watanzania wanaopenda kuwekeza kwenye zao hili ili kujitosheleza.

"Kwa sasa matunda yamekwisha na soko limefunguka, wanunuzi wanakuja na mamilioni ya pesa na kurudi nayo kwa sababu matunda hakuna ila Njombe tuna ardhi ya kutosha," alisema Msigwa.

Baadhi ya wakulima wa parachichi mkoani Njombe akiwamo Godfrey Nyagawa, walipongeza kuanzishwa kwa mfumo huo wa kuwasaidia wakulima wanaovutiwa kuwekeza katika kilimo cha maparachichi huku wakisema utasaidia kukuza uchumi wa familia na mkoa kwa ujumla kutokana na uhitaji mkubwa wa zao hilo.

"Programu hii itasaidia sana kukuza uchumi kupitia kwenye kilimo hiki hususani kwenye familia. Lakini itaongeza uzalishaji wa zao hili kwa kufanya matunda yaongezeke kwa wingi kwasababu hayatoshelezi kwa sasa," alisema Nyagawa.

# Wafanyabiashara waamriwa kuondoka eneo la barabara, kurudi walikopangiwa

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, ameagiza wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao katika eneo la hifadhi ya barabara kuondoka na kurudi katika eneo walilopangiwa katika soko la Msufini, Picha ya Ndege.

Msafiri alitoa agizo hilo jana alipotembelea soko la Msufini na kubaini wafanyabiashara wengi wakiendelea kulitelekeza soko hilo na kufanya shughuli zao katika hifadhi ya barabara.

Eneo hilo la hifadhi ya barabara ni finyu na hatari kwa maisha yao kutokana na mchanganyiko wa biashara zinazofanyika na ukosefu wa huduma muhimu kama vile vyoo na maji.

"Niwaombe wafanyabiashara wanaoendelea kufanyabiashara soko la Picha ya Ndege kando ya barabara waje hapa isipokuwa mama lishe, wachoma chipsi na bodaboda wataendelea kutoa huduma kwenye eneo hilo," alisema.

Msafiri ambaye aliongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, alitumia fursa hiyo kuwataka wafanyabiashara kushirikiana, kusimamia makubaliano wanayoafikiana, kuheshimu uongozi uliopo kisheria, kuacha malumbano na siasa chafu na kufanya biashara kwenye maeneo yaliyopangwa.

Alisema kama wafanyabiashara hao hawatachukua uamuzi wa kuhamia eneo la soko lililotengwa, serikali haiko tayari kutoa mikopo kwa watu wasiojulikana wanakofanyia biashara.

Awali, akimkaribisha Mkuu wa Wilaya kuzungumza na wananchi, Diwani wa Sofu ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashaurinya Mji Kibaha, Mussa Ndomba, alisema soko hilo lina miundombinu ya umeme, maji na huduma safi za vyoo.

Ndomba alisema soko hilo lina uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 526 kwa sasa na limetoa fursa kwa wafanyabiashara wengine kutoka nje ya kata hiyo kulinganisha na soko la awali lililokuwa na uwezo wa wafanyabiashara 150.

Kabla ya kufika katika Soko la Msufini, Msafiri alitembelea wafanyabiashara wa masoko ya Mnarani na Mailimoja wanaofanya shughuli zao majira ya jioni katika eneo la hifadhi ya barabara ambalo halijaendelezwa na kuwataka kuzingatia sheria kuondoa mgongano na serikali.



Meneja Mikopo wa Benki ya NBC makao makuu, Mtenya Cheya, akizungumza na wastaafu watarajiwa kutoka taasisi za serikali na mashirika binafsi wakati wa semina iliyoandaliwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), na kudhaminiwa na wadau mbalimbali ikiwamo benki hiyo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yazindua akaunti mpya ya jamii

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imezindua rasmi huduma mpya ya kibenki ijulikanayo kwa jina 'NBC Jamii Akaunti' ambayo ni mahususi kwa ajili ya taasisi zisizo za kiserikali (NGO), taasisi zinazotegemea misaada, zinazotoa misaada kwa jamii na taasisi za kidini.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa huduma hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa Huduma hiyo, Mwinyiusi Hamza, alisema 'Jamii Akaunti' inalenga kuzaisaidia taasisi hizo ili kupata huduma za kibenki bila makato yoyote.

"Kupitia 'NBC Jamii Akaunti', NGO na taasisi zinazotegemea misaada kwa sasa zitapokea, kutunza fedha za miradi toka kwa wahisani bila makato ya mwezi huku zikifuatilia kila muamala unaofanyika.

"Pia kwa upande wa taasisi za kidini kwa maana ya makanisa na misikiti kupitia 'NBC Jamii Akaunti' kutakuwa na urahisi zaidi wa upokeaji wa sadaka na zaka pamoja na michango mingine bila kusahau utunzaji wa fedha za miradi toka kwa wahisani na wadhamini wa taasisi hizi za kidini," alisema.

Hamza alisema wadhamini, waumini na wahisani wanaweza kuweka fedha moja kwa moja kwenye akaunti ya NBC Jamii ya taasisi husika kupitia njia mbalimbali na rahisi ikiwamo kutumia huduma ya NBC Kiganjani kutoka kwenye akaunti ya mtoaji kwenda moja kwa moja kwenye akauti ya taasisi husika.

"Pia wanaweza kuweka fedha zao kupitia ATM za NBC zinazopokea fedha na kuweka moja kwa moja kwenye akauti ya taasisi husika ya NBC Jamii. Pia wanaweza kutumia mawakala wa NBC (NBC Wakala) na kuweka fedha hizo moja kwa moja kwenye akaunti ya taasisi husika ya NBC Jamii. Njia nyingine ni pamoja na kutumia matawi yetu pamoja na simu za mikononi," alisema.

Kuhusu baadhi ya faida za akaunti hiyo kwa walengwa, Mkuu wa Kitengo cha Wajasiriamali cha NBC, Mussa Mwinyidaho, alisema pamoja na mambo mengine inawarahisishia wamiliki wa akaunti ufuatiliaji wa vitabu vya taasisi husika kupitia rekodi ya miamala isiyoingiliwa na makato.

"Zaidi kupitia akaunti hii wamiliki wanaweza kufanya malipo kwa watu wengi kwa mara moja kupitia huduma ya 'NBC Business Internet Banking'. Pia wanaweza kupokea taarifa za miamala ya fedha inayoingia na inayotoka sambamba na kupatiwa kitabu cha hundi bure," aliongeza.

# ZFDA yataka ukaguzi wa bidhaa mara mbili

**Na Mwandishi Wetu**, PEMBA

WAKALA wa Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA) Ofisi ya Pemba, imependekeza kufanyika uchunguzi kwa mara ya pili wa bidhaa zinapofika kisiwani hapa ili kuepusha kuharibika au kufanya udanganyifu.

Akizungunza na mwandishi wa habari hii baada ya kuzuiwa mchele aina ya Sunflower Rice kwenye meli ya Sea Star 1 Julai 10, mwaka huu kutoka Unguja, Mkurugenzi wa ZFDA Pemba, Nassir Salum Buheti, alisema ni vyema bidhaa zinapofika Pemba zifanyiwe tena uchunguzi wa mara ya pili.

Alisema bidhaa nyingi huharibika ghalani au kufanyika udanganyifu wa kuweka bidhaa mbovu kwenye vifungashio vipya, hivyo kuna haja ya kufanya uchunguzi kwa mara ya pili na kuchukuliwa sampuli kila baada ya miezi mitatu ili kuepuka udanganyifu.

"Wafanyabiashara wanafanya udanganyifu na kuwalisha wananchi vyakula vibovu hali ambayo inaweza kuhatarisha maisha yao. Tunapendekeza kufanyiwa uchunguzi wa mara ya pili bidhaa zinazoingia Pemba hasa za mchele. Hii itasaidia kulinda afya ya mlaji," alisema.

Alisema mchele huo uliofika Bandari ya Wete Julai 10 polo 400 wenye ujazo wa kilogramu 50 kwa kila moja, ambao ni mali ya wafanyabiashara Abdi Abdalla na Saleh Mbarouk Kombo. Baada ya kupelekwa maabara, mchele huo uligundulika kuwa haufai kwa matumizi ya binadamu.

Baada ya kupata majibu hayo, alisema ZFDA makao makuu iliamua kwenda kuchukua sampuli nyingine ya mchele huo ghalani mwa mwagizaji kwa ajili ya uchunguzi na kubainika kuwa pia haufai.

Mkurugenzi huyo alisema baada ya kuona mchele huo haufai kwa matumizi lakini ulishaingizwa sokoni, walitengeneza timu ya ukaguzi kwa ajili ya kuhakikisha unazuiwa kutumika na kufanikiwa kuzuia polo 1,018 katika maeneo mbalimbali kisiwani Pemba na kupanga utaratibu wa utekelezaji.




Wageni rasmi mnatuzingua bhana!

Ukurasa 13

**Corona inavyokimbiza watalii Zanzibar**

Ukurasa 14




# BUFE

Ijumaa Agosti 6, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


BIASHARA

# Vijana wajipanga kupigania uchumi kupitia mlango wa bidhaa usindikaji

## • YPC kijana njia za 'pa kutokea'

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

SEKTA ya kilimo ina mchango mkubwa katika uchumi na maendeleo Barani Afrika. Sekta hiyo ni chanzo kikuu cha chakula kwa watu zaidi ya milioni 950 wanaoishi katika nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara na malighafi zinazotumika viwandani

Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia, mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa kwa Nchi hizi ni asilimia 15. Aidha, nchi ya Afrika ya Kusini, ndiyo yenye mchango mkubwa zaidi wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa, wa asilimia 50.

Kwa upande wa Tanzania, baadhi ya manufaa ya sekta ya kilimo ni pamoja na kutoa mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 27.5, chanzo kikuu cha ajira kwa kuajiri zaidi ya asilimia 65 ya nguvu kazi na chanzo kikuu cha fedha za kigeni kwa kuingiza wastani wa asilimia 24.7 ya fedha, zitokanazo na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa ya mtakwimu mkuu wa Serikali Ofisi ya Taifa ya Takwimu zilizotolewa baaada ya kufanyika Sensa ya Tano ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Mwaka wa Kilimo 2019/2020.

Watanzania wengi wanajishughulisha katika Sekta ya Kilimo na wanahusika kuzalisha mazao wakiyauza ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, mazao wanayoyazalisha yamekuwa yanakosa soko na mengine yanaelezwa kuharibika kwa kutokuwa na viwanda vya kutosha kuchakata mazao hayo kwa wakati.

**WAZALISHAJI VIJANA**

Mkurugenzi wa Asasi ya Vijana ya YPC Israel Ilunde, anaelezea namna wanavyotoa elimu kwa vijana waweze kujikita kwenye Sekta ya Usindikaji badala ya kusubiri ajira.

Ilunde anasema katika hatua za awali wametafakari hali halisi ya Sekta hiyo ya usindikaji wa vyakula na kuwahamasisha Vijana kujikita huko.

"Baada ya kutafakari suala la ajira tulienda zaidi kwenye ukosefu wa ajira hata ajira zikipatikana ni vizuri kuangalia na ajira yenyewe kazi zenye staha ndani ya Sekta ya usindikaji wa vyakula" anasema Ilunde



Kiwanda cha kisasa cha uchinjaji na usindikaji wa nyama cha Tan Choice kilichopo Soga, wilayani Kibaha mkoani Pwani. **PICHA MTANDAO.**

Katika hatua ya awali, anasema wamewakutanisha vijana na kuzungumzia sekta hiyo ya usindikaji kupitia kilimo, ili yeyote anayejihusisha nayo iwe ni kazi yenye staha.

Ilunda anasema, usindikaji wote unategemea mazao kutoka mashambani hivyo kama Kilimo kitadorora usindikaji tadorora pia .

"Tumelenga kilimo kwa kuwa ndio kinacholeta unafuu wa maisha, asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea mazao kutoka shambani, hivyo vijana wenye nguvu wanatakiwa waingie shambani wazalishe mazao na wengine wanunue na kusindika baadae waviuze ndani na nje ya nchi na kujikwamua kiuchumi," anafafanua.

Anasema, kazi ya usindikaji vyakula ina mapokeo madogo kwa vijana, hivyo kwa sasa wanatakiwa kubadilika kuhamishia mawazo yao kuchakata mazao na kutafuta masoko ndani na nje ya nchi.

"Walimu wa stadi za kazi waanze kuwafundisha wanafunzi wa shule ya msingi kulima bustani waandaliwe kujikita katika sekta hii ya kilimo, tukianzia chini mabadiliko makubwa yataonekana baadae na hakutakuwa na malalamiko ya ajira" anasema

Ilunmda anafafanu, kwa sasa wanawake wanaongoza kwenye sekta ya usindikaji vijana bado ni wachache na sasa kundi la wanawake wanatakiwa kuanza kuwafundisha ili nao watumie fursa hiyo kujiajiri.

Katika kongamano la vijana lililoandaliwa na YPC, walipitisha mapendekezo ya kuwa sekta ya usindikaji unaotegemea sekta ya kilimo.

Hivyo, anasema kilimo kilipewa umuhimu unaostahili kitaifa na kuwekewa mazingira mazuri ili wasindikaji vyakula wafanye kazi zenye staha na kuwa na matokeo bora

Mapendekezo mengine ambayo yaliwasiliahwa na Mkurugenzi wa YPC ni pamoja na sekta ya usindikaji itambuliwe kama mwajiri mama na itungiwe sera itakayosaidia namna ya kuzalisha ajira zenye staha kwa vijana

Nyingine ni wanaoanzisha kampuni au miradi katika sekta ya usindikaji, wapewe motisha na kuungwa mkono na serikali, pia wadau wote kuepuka vizuizi vya kuanzisha na kuendesha shughuli za usindikaji

Pendekezo lingine, ni nguvukazi ya Taifa husuan wahitimu wa elimu ngazi mbalimbali waandaliwe na taasisi mbalimbali ikiwamo Vyip vua Ufundi Stadi (VETA), ili waweze kuajiriwa na sekta ya usindikaji.

Mweleke mwingine ni kwa vijana wanaojishughulisha na usindikaji wa vyakula wawezeshwe kifedha, kiteknolojia na masoko ili kazi ziwe zenye staha na zilete tija.

Ilunde anawataka Maofisa Maendeleo ya Jamii pamoja na Maofisa Maendeleo ya Vijana, waongeze juhudi ya kuwasaidia vijana wawasaidie vijana waliopo katika sekta ya usindikaji, ili wafanikiwe zaidi hata kuweza kuwaajiri vijana.

"Pendekezo letu lingine ni serikali kupitia jumuiya za kikanda na za kimataifa ihakikishe kuondolewa kwa vikwazo vya kuvuka mipaka wakati wa kufanya biashara ya bidhaa za usindikaji, ili kupanua masoko na kubadilishana uzoefu na mataifa mengine juu ya tasnia na bidhaa zitokanazo na usindikaji" anabainisha.

# Kiama Mlima wa Lyamba lya Mfipa kinavyoondoshwa

## • Wanasheria, RUSUDEO wanavyohamasisha wananchi usimamizi endelevu wa maliasili

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA ni miongoni mwa mataifa yaliyosheheni maliasili za kila aina kuanzia misitu, mito, maziwa, ardhi, madini na wanyamapori zinazovutia watalii na uwekezaji kwenye uzalishaji mali.

Ripoti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya mapato na matumizi kwa mwaka 2018/2019, inaonyesha kuongezeka idadi ya watalii kutoka 1,284,279 walioingia nchini mwaka 2016 hadi 1,327,143 waliotembelea Tanzania 2017, likiwa ni ongezeko la asilimia tatu

Rukwa ni moja ya mikoa iliyosheheni rasilimali nyingi hapa nchini ambazo zinazotoa fursa kwa maendeleo ya watu, kuvutia utalii na kutunza ikolojia katika wilaya za Nkasi, Sumbawanga na Kalambo na maeneo jirani.

Safu za milima ya Lyambalya Mfipa ina misitu ambayo ni chanzo cha dawa asilia na pia hutunza Utamaduni wa wana wa Rukwa.

Aidha, uwepo wa maziwa Rukwa na Tanganyika, Mlima Chala, mabonde na makaa ya mawe, maporomoko ya Kalambo, wanayama katika pori la Lukwati , pori Tengefu la Uwanda ambalo ni asilimia 80 ya Ziwa Rukwa na ardhi yenye rutuba ni tunu za utajiri mkoani humo.

Huwezi kutaja kukua uchumi wa wananchi wengi wa Rukwa bila kuzungumzia tunu hizo. Kwa mfano takwimu za mkoa huo za kipindi cha 2018/2019 zinaeleza kuwa tani 2,976.75 za samaki zenye thamani ya Sh. bilioni 12.9 zilivunwa na kusafirishwa ndani na nje ya mkoa huo.

Aidha, wananchi 14,094 wanajishughulisha moja kwa moja na uvuvi, wakati 1,021 wanajikita kwenye uchakataji wa mazao ya uvuvi huku 2,820 wakimiliki mitumbwi.

Pamoja na faida lukuki za ardhi, misitu, wanyamapori na maji usimamizi wa rasilimali hizi unazungukwa na changamoto nyingi hivyo kufifisha fursa za wananchi na ustawi wa mali asili hizo.

Kwa mfano Ofisa Ardhi ambaye ni Mkuu wa Idara ya Maliasili wa Wilaya ya Nkasi, Pasian Assenga, anaiambia Nipashe kuwa takribani hekta 1,000 za msitu wa Lyamba lya Mfipa huvunwa kwa njia haramu.

Kwa mujibu wa utafiti wa awali wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili, wananchi wengi wanafua na kufanya shughuli mbalimbali katika vyanzo vya maji na kuchafuka mito mambo yanayodhuru watumiaji wengine hasa wanaoishi kuzunguka milima ya Lyamba lya Mfipa.

Taarifa ya utafiti inasema athari hizo zimewaumiza zaidi wananchi walioko chini ya milima hiyo kuliko wakazi wa Nkasi waliopo upande wa juu wa milima hiyo. Hii ni kutokana na jiografia ya tarafa ya Mtowisa katika Wilaya ya Sumbawanga inayopatikana upande wa mashariki mwa Wilaya ya Nkasi ambayo iko bondeni kuelekea Ziwa Rukwa, hivyo kupokea taka na uchafu unaotoka milimani.

**KUDHIBITI TATIZO**

Assenga anasema ni lazima kulidhibiti, akitaja magonjwa yanayowasumbua wananchi upande wa chini wa safu ya Milima ya Lyamba Lya Mfipa kuwa ni changamoto kiafya kwa wanashambuliwa na maradhi kama tumbo na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu kilichotokea Mei 2018 na kusababisha wagonjwa 109 na vifo vinne kuripotiwa.



Ndivyo wananchi wanavyochafua mazingira na vyanzo vya maji na kuhatarisha afya za wanaoishi mabondeni na hatma ya safu za Mlima Lyamba lya Mfipa. **PICHA: LEAT**

Kutokana na hitaji la kuendelea kutunza mazingira na maliasili zilizo katika milima ya Lyamba Lya Mfipa, Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT) kwa kushirikiana na Taasisi ya Maendeleo Endelevu Rukwa (Rukwa Sustainable Development Organization)-RUSUDEO inatekeleza mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili.

Taasisi hizo zinafanyakazi katika vijiji 15 vya tarafa za Chala, Kate na Mtowisa pamoja kata za Nkandasi, Mkwamba, Kipande, Muze, Kalumbaleza na Mwadui kwa kushikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (USAID).

Maeneo hayo yanazunguka milima ya Lyamba lya Mfipa iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

Mkurugenzi Mtendaji wa LEAT, Dk. Rugemeleza Nshala, anasema mradi huo utatekelezwa kwa miaka mitano kuanzia Machi, 2020 hadi Machi, 2025.

Aidha ni moja ya jitihada za kuunga mkono hatua zinazochukuliwa na serikali katika kusimamia rasilimali za maliasili hususani ardhi, maji, wanyamapori na misitu katika Mkoa wa Rukwa, anasema Dk. Nshala.

LEAT na RUSUDEO wanalenga kuhamasisha usimamizi endelevu wa maliasili ili kutatua changamoto za kiuhifadhi zinazoikabili Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi na Sumbawanga.

"Ni dhahiri kuwa pamoja na faida lukuki za ardhi, misitu, wanyamapori na maji bado usimamizi wa rasilimali hizi unakabiliwa na changamoto nyingi hivyo kuzorotesha fursa za wananchi na ustawi wa rasilimali," anasema Mkurugenzi wa LEAT

Moja ya vyanzo vya maji, kwa mfano, vinaendelea kuvamiwa na wakulima na wafugaji, kuongezeka kwa sumu na vimelea vya magonjwa katika vyanzo vya maji na mmomonyoko wa udongo pembezoni mwa vyanzo hivyo, anasema.

Anakumbusha kuwa shughuli hizi za kibinadamu zinazofanywa katika hifadhi za misitu na vyanzo vya maji zinaenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya 2004 la kutofanyika kwa shughuli za binadamu ndani ya mita 60 kutoka kwenye kingo za mito, maziwa, bahari, bwawa la maji au hifadhi ya maji.

Baadhi ya wakazi wa maeneo yaliyoathirika kutokana na uharibifu wa mazingira, wanasema kuvunjika kwa madaraja ya tarafa ya Mtowisa Wilaya ya Sumbawanga ni kielelezo cha namna mabadiliko ya tabianchi na uvunaji mazao ya misitu usiofuata taratibu ulivyo mbaya kwa ustawi wa watu na ulinzi wa mali zao.

LEAT inaamini katika ushirikishwaji wa jamii kufikia utawala bora wa maliasili hivyo ni lazima jamii iwezeshwe katika kupata maarifa na zana za usimamizi wa maliasili zao. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kifungu cha 187, inakataza kuchafua mazingira ndiyo ndiyo muktadha huo, LEAT inatazamia kutoa elimu kwa wadau juu ya kanuni, taratibu na sheria za uhifadhi wa maliasili, kuratibu utengenezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, kusaidia kuongeza uelewa na ufahamu wa kamati mbalimbali wilayani humo.

Kamati hizo zitaelimishwa juu ya usimamizi endelevu wa maliasili na ufuatiliaji wa uwajibikaji jamii, kuratibu utengenezwaji wa sheria ndogo, upandaji miti na kufanya kazi na vikundi vya kijasiriamali katika kata sita za mradi.

Mkurugenzi Mtendaji wa LEAT, Dk. Nshala katika mkutano wa uzinduzi wa mradi uliofanyika hivi karibuni, anahimiza ushirikiano kutoka kwa wadau, watendaji wa kata na vijiji vya mradi, viongozi na watendaji wa halmashauri za wilaya za Nkasi na Sumbawanga.

'Mradi huu si wa kisiasa, siasa yetu ni kuhifadhi maliasili kwa misingi dumivu na endelevu na kushirikiana na wananchi kwa pamoja ili kuwawezesha kutunza maliasili zao kwa misingi inayoeleweka'" anasema Dk. Nshala.

Andy Karas, Mkurugenzi Mkazi wa USAID Tanzania, anasema kuwa USAID inajivunia kufanya kazi na LEAT kupitia mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili.'

"Bado tunaheshimu ushirikiano huu na ni matarajio yetu kuwa ushirikiano huu utazidi kuwa mkubwa huko mbeleni."

Anasema mradi huu utaendeleza ushirikiano baina ya Serikali za Marekani na Tanzania, kwenye uhifadhi wanyamapori, misitu na vyanzo vya maji katika mfumo wa Ikolojia wa Lyamba lya Mfipa.

"Utajiri wa uhainuai wa Tanzania unakabiliwa na changamoto nyingi kama vile uvunaji haramu wa miti na uchafuzi wa vyanzo vya maji. Changamoto hizi zinathibitisha uwezo duni wa mamlaka za serikali za mitaa katika kusimamia vyema utunzaji wa maliasili na kupelekea matokeo duni ya uhifadhi wa maliasili na hivyo kuhatarisha jamii zinazozunguka," anaeleza Karas.

---

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wageni rasmi mnatuzingua bhana!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

HIVI hii dhana ya mgeni rasmi au mgeni wa heshima, ilitoka wapi? Nini asili yake? Au ni yale yale yatokanayo na utamaduni wa kigeni?

Unakuta mahali eti kuna jambo linaweza kufanywa na mwenyeji pengine ni kijijini, katani, tarafani, wilayani au mkoani, lakini halifanyiki kwanza mpaka mgeni rasmi au mgeni wa heshima afike!

Tena wakati mwingine mtatangaziwa kuwa mgeni rasmi atafika saa 4:00 asubuhi, hivyo wananchi fikeni eneo la tukio kuanzia saa 1:00 asubuhi. Cha kushangaza, mgeni anaweza kufika saa 11 jioni.

Mmekaa hapo, kwanza hamjafungua vinywa kwa sababu ya kuchelea kuharibu ratiba ya mgeni rasmi. Mmepigwa jua na hata kunyeshewa mvua kama si kupigwa vumbi au baridi, kutegemea eneo husika.

Jambo lenyewe pengine ni la kufungua, kuzindua au kuweka jiwe la msingi! Mambo ambayo hata asipofika jambo hilo litafanyika tu. Kwani lisipozinduliwa au kufunguliwa, darasa halijengwi maadam kuna matofali na wajenzi?

Lakini mtahangaishwa wee, wakati mwingine hata watoto wasiende shule kwa sababu anakuja mgeni rasmi kutoka mkoani au taifani kuzindua, kuweka jiwe la msingi au kufungua mradi.

Inachosha, inaumiza, inakera na ina ukakasi kwa kweli. Jambo linaweza kuwa zuri tu tena lenye faida, lakini watu wanapoteswa na mgeni rasmi au mgeni wa heshima kwa kuchelewa kwake, hugeuka kero na kuchukiwa.

Hivi sasa Tanzania imeanza chanjo dhidi ya UVIKO-19 tena kwa hiyari, wanaojitokeza wanafanya hivyo, walioapa kwamba hawataki kusikia kamwe, pia wapo na hawapelekewi mbwa wa polisi nyumbani kuwalazimisha, wala mabomu ya kutoa machozi.

Nchi iko huru na ina demokrasia na kila mwenye lake anasema na anafanya bila kubughudhiwa. Lakini kuna mahali eti chanjo nayo ina ugeni rasmi! Jamani hebu tuache hizo. Mtu anasubiriwa kuzindua chanjo, wachanjwaji wakimsubiri.

Si porojo, juzi kati nilishiriki chanjo tena naiamini tu. Tukaitwa pale Karimjee, Dar es Salaam, kuchanja tena kwa lifti ya wake za viongozi, wake za vigogo, lakini karibu wengi niliowaona pale ni wa vigogo wastaafu.

Nikawatambua Mama Tunu Pinda, nikamwona Mama Kawawa, nikamwona Mama Januari (Makamba). Akawepo Mama Mary Majaliwa, huyu ndiye alikuwa mgeni wetu rasmi wa chanjo.

Tulikuwa tumetangaziwa kuwa tufike pale kuanzia saa 1:30 asubuhi, ili tufanye chapchap tuendelee kufukuzia Shilingi iliyoota matairi mtaani, kupitia vibarua vyetu. Yaani chanja ukimbilie riziki mtaani.

Tukawa tumejilawa wachanjwaji, kufika hapo tukasondekwa ndani ya ukumbi uliokuwa wa mikutano ya bunge, watu pomoni, mkusanyiko usio wa lazima, barakoa kwa kwenda mbele, lakini hewa nzito. Kaa, kaa na wewe, subiri, subiri na wewe.

Emsii akawa anaendelea kututia moyo, kuwa baada ya vijidakika hivi mgeni rasmi, Mama Majaliwa atakuwa anaingia ili kutuzindulia chanjo. Nikajiuliza hivi chanjo hii iliyokwishazinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan ina haja ya kuzinduliwa tena?

Kaa, kaa na wewe, subiri, subiri na wewe. Baada ya kama saa nne kupita hivi likaingia Vieite jeusi akashuka mama akaingia ukumbini, tukasimama kama ilivyo ada kumlaki mgeni rasmi.

Emsii akapanda kunako ulingo na kututangazia ujio wa mgeni rasmi na kutambulisha waliko wake za viongozi, tukashangilia kama kawaida yetu wachanjwaji. Tukajua sasa mambo yameiva tunaanza.

He! Ratiba ikasomwa kuwa ataanza nanihii kuhutubia, atafuata nanilii, kisha naniliu na baada ya hapo atapanda huyu ninihii na kisha atafuata nanihii na hatimaye akimaliza naniliu huyu atamkaribisha mgeni rasmi.

Mh, nikaona sasa watu wanaanza kutazama simu zao, bila shaka si kusoma ujumbe, bali kuangalia ni saa ngapi ili wakimbizane na shilingi. Wengine wakaona isiwe tabu wakajitoa mchezoni. Walipomaliza hotuba, wakachanjwa walengwa wa awali, wake. Wakaondoka.

Tukabaki tukachanja. Ngoma sasa. Vyeti vya kuthibitisha ulichanja, hola! Emsii tena, jamani subirini vyeti vinakuja vimechelewa kidogo! Nikajiuliza, mgeni rasmi kachelewa na vyeti vimechelewa, hawakujiandaa? Hii ndiyo Bongo isiyo na haraka. Mwendo wa jongoo na vumbi nyuma. Alamsiki!

# Corona inavyokimbiza watalii Zanzibar

## • Shule zakosa misaada, wazazi kipato

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ULE msemo wa wahenga 'mgeni njoo mwenyeji apone"sasa umeingia mushkeli, baada ya kuzuka janga la ugonjwa wa corona.

Zanzibar, ni moja ya sehemu zinazotembelewa na idadi kubwa ya watalii, ikinufaika na mchango wao kwa maendeleo ya sekta za kijamii na hasa afya na elimu.

Watalii walikuwa wanasaidia maendeleo ya shule wanapofika katika vijiji vyenye fukwe nzuri za kitalii kwa ajili ya kutembea.

Baadhi ya shule ziliweka visanduku maalum kwa ajili ya maendeleo ambapo watalii wanaofika katika maeneo hayo huweka fedha kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya shule husika.

Fedha hizo zilikua zikisaidia maendeleo ya shule husika ikiwemo ununuaji wa vifaa kwa ajili ya kutoa elimu bora kwa wanafunzi.

Kwa mfano kila mwaka Karin Khan, alikuwa akifika Zanzibar kwa ajili ya utalii na anatembelea visiwa hivi kwa zaidi ya miaka 15 sasa kiasi cha kumfanya kuwa mwenyeji wa Zanzibar lakini kwa sasa amesita kuja kwa sababu ya janga la corona.

Alipokuja kwa mara ya kwanza kama mtalii yeye na mume wake zaidi ya muongo mmoja sasa, Karin alipendelea kuishi katika vijiji vya Uroa na Marumbi Wilaya ya Kati Unguja.

Vijiji hivi ni moja ya sehemu yenye uwekezaji mkubwa wa sekta ya utalii, ambayo kabla ya janga la COVID-19 lililoikumba dunia mwaka 2020, ilikuwa ikichangia zaidi ya asilimia 27 ya pato la taifa.

Wakati akiwa katika vijiji hivi, Karin alipendelea kutembelea shule za sekondari za Uroa na Marumbi ambapo alipata nafasi ya kubadilishana mawazo na walimu na wanafunzi.

Baadae alivutiwa na shule hizi hasa kutokana na ukarimu wa walimu na wanafunzi wake na kuanza kuzisaidia.

Alitumia kila fursa aliyoipata nyumbani Ujerumani kusaidia shule hizi kuanzia ujenzi wa vyumba vya kompyuta, uwanja wa michezo, vitabu, huduma za maji, vifaa vya maabara na miundombinu mengine muhimu kwa maendeleo ya shule.

Kwa wanafunzi wa shule hizi kwake walikuwa kama watoto wake. Alihakikisha wanasoma katika mazingira mazuri ili wapate elimu bora itakayowasaidia katika maisha ya baadae.

Sera ya elimu ya Zanzibar ya mwaka 2003 inatoa fursa kwa wazawa na wageni kuchangia maendeleo ya sekta ya elimu ingawa jukumu lipo kwa serikali.

Nilipokutana nae kwa mara ya mwisho mwaka 2019, Karin aliahidi kuendelea kusaidia maendeleo ya shule hizo kwa sababu aliamini elimu ndio msingi bora wa maendeleo.

Kwa shule zilizopo ukanda wa pwani, watalii walikuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya shule hizo.




Biashara ya vyakula eneo la Forodhani visiwani Zanzibar ni moja ya mambo yanayovutia watalii. **PICHA: MTANDAO.**

> **"Asilimia 99.4 ya wageni walikuja kwa ajili ya mapumziko, asilimia 0.5 kwa ajili ya kuwatembelea ndugu na marafiki zao na asilimia 0.1 ya wageni walikuja kwa sababu nyingine**

Kila shule ilikuwa na kisanduku cha kuhifadhi fedha kilichojengwa nje ya shule na katika miradi ya utalii, kikiwa na ujumbe 'Changia maendeleo ya elimu'.

Watalii waliotembelea vijiji hivi walipata fursa kuchangia kwa hiari maendeleo ya sekta ya elimu ya vijiji hivyo.

Ali Kituwa ambae aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Marumbi, anasema watalii walikuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya shule hiyo na nyengine za ukanda wa pwani.

Janga la COVID-19, hata hivyo, limesimamisha kila kitu.

Michango ya watalii kwa maendeleo ya shule hizi imekatika kwa sababu ya kuenea maambukizi ya ugonjwa huo duniani kote yaliyosababisha mataifa mengi kusitisha shughuli za utalii.

"Walikuwa wakichangia dola na baadae tunazibadilisha kwa fedha ya Tanzania kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ya shule yetu. Sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo ya shule yetu ilizibwa na fedha za michango kutoka kwa watalii," alisema Kituwa.

"Tulikuwa tukibadilisha hadi dola 3,000 kwa mwezi. Katika maisha yangu yote, haijawahi kuwa kama hii. Kulikuwa na watalii kila wakati,"alisema.

"Sasa hakuna watalii, hakuna dola kwa sababu ya COVID-19. Sasa tunategemea ruzuku kutoka serikalini pekee ambayo hata hivyo haitoshi na haipatikani kwa wakati, "alisema.

Nassra Ali mwanafunzi wa Shule hiyo alisema, kabla ya janga la Corona, Shuleni kwao walikuwa wakipokea watalii mbalimbali wenye lengo la kuwasadia katika masomo yao.

"Wapo ambao waliokua wakitupa msaada wa vifaa mbalimbali vya Shule lakini pia wapo ambao waliokuwa wakijitolea kutufunza lugha za kigeni kwa muda wa masomo ya ziada,"alisema.

Alisema ujio wao umesaidia kuinua kiwango chao cha ufahamu hasa kwa somo la Kiingereza.

Virusi vya corona vimeangamiza tasnia ya utalii ya Zanzibar iliyokuwa ikichangia mamilioni ya dola kwa mwaka na kuacha makumi ya maelfu ya watu kutoka kisiwa hiki maarufu barani Afrika- wakihangaika.

Zahor Ali (sio jina lake halisi) anafundisha Shule ya Sekondari ya Jambiani, moja ya shule iliyozungukwa na hoteli za kitalii kusini mwa kisiwa cha Unguja.

Zahor anasema, watalii waliotembelea kijiji hicho kinachosifika kwa fukwe zenye mchanga mweupe, walikuwa na mchango muhimu kwa maendeleo ya shule.

"Lakini sasa kila kitu kimebadilika, hakuna mapato yanayoingia kwa sababu watalii hawaji kwa wingi," alisema.

Hata hivyo, ana matumaini kwamba hali inaweza kurejea kama zamani kama ugojwa wa COVID-19 utadhibitiwa.

"COVID-19 imeathiri kila sekta ikiwemo ya elimu, tulikuwa tunatembelewa na watalii mara kwa mara katika skuli yetu na wengine walikuwa wakichangia fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za shule," alisema.

"Kwa kawaida huu ndio ulikuwa msimu wa shughuli nyingi zaidi utalii kwa mwaka. Mikahawa na hoteli zinakuwa zimejaa, lakini COVID-19 ilitokea na kila kitu kikaharibika,"alisema Zahor.

Aliendelea kwa kusema:"Virusi vya corona imeharibu uchumi wa eneo hilo na vimesababisha akaunti ya benki ya shule yetu kuwa tupu. Hakuna mtu katika jamii alieokoka na corona."

TAKWIMU

Watalii 20,416 wamewasili Zanzibar kwa mwezi wa Juni mwaka huu ambapo kwa Mwezi wa Machi, Mwaka huu waliongia nchini walikuwa 9,280.

Akitoa takwimu za uingiaji wa wageni kwa waandishi wa habari Ofisini kwake Mzazini, Mkuu wa Idara za Takwimu za kiuchumi, kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali,Abdulrauf Ramadhani Abeid, alisema Ufaransa inaongoza kwa kuleta watalii wengi Zanzibar.

Alisema jumla ya wageni 11,588 walioingia nchini kutoka Bara la Ulaya sawa na asilimia 56.8 ya wageni wote wa mwezi wa Juni, mwaka huu.

Alisema kwa mwezi huo wa Juni Ufaransa iliongoza kwa kuleta wageni 2,232 sawa na asilimia 10.9 ya wageni wote ikifuatiwa na Polish 2,101 sawa na asilimia 10.3.

Alieleza kuwa wageni waliongia Zanzibar kwa kutumia usafiri wa boti kupitia Bandari ya Malindi walikua 5,152 sawa na asilimia 25.2 na waliongia kupitia viwanja vya ndege ni 15,264 sawa na asilimia 74.8.

"Asilimia 99.4 ya wageni walikuja kwa ajili ya mapumziko, asilimia 0.5 kwa ajili ya kuwatembelea ndugu na marafiki zao na asilimia 0.1 ya wageni walikuja kwa sababu zengine", alisema Abeid.

Naye, Dk. Estella Ngoma Hassan, Muhadhiri kutoka Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), alisema kuwako na idadi kubwa ya wageni kutoka Ufaransa imetokana na nchi hiyo kuondosha vikwazo vya kusafiria katika nchi yao na kusababisha kuondoka nchini na kwenda nchi zingine hali iliyopelekea Zanzibar kupata wageni wengi kutoka nchini humo.

Aidha alisema kuwa sababu nyingine iliyopelekea wageni kutoka Ufaransa kuwa wengi Zanzibar ni pamoja na kuanza zoezi la chanjo ya Corona nchini humo.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Dk. Abdulla Mohammed Juma, alisema kamisheni hiyo imebadilisha mikakati ya soko la utalii ambapo awali walikuwa wakitegemea watalii kutoka ulaya.

Hivyo alisema kuwa kupitia mikakati hiyo imeanza kuzaa matunda ambapo wageni mbalimbali wamekuwa wakiongezeka.

Aidha anaeleza kuwa kwa miaka sita iliyopita nchi iliyokua ikiongoza kuleta watalii kwa wingi Zanzibar ni Italia ambapo hivi sasa idadi imepungua kutokana na janga la corona.





# Wanaonyonya maziwa ya wake zao waonywa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WANAUME wanaonyonya maziwa ya wake zao wanaonyonyesha wametakiwa kuacha tabia hiyo kwa sababu inaweza kuwa chanzo cha magonjwa ya kuambukiza kwa watoto wao.

Ofisa Lishe kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Tufingene Malambugi, alitoa onyo hilo juzi wakati wa warsha kwa waandishi wa habari kuhusu Maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama Duniani iliyofanyika jijini hapa.

Malambugi aliwaonya wanaume wenye tabia hiyo ya kunyonya maziwa ya wake zao wanaonyonyesha kuacha kwa sababu inachangia kusababisha maambukizi kwa watoto wao.

"Ninatoa onyo kwa wanaume wenye tabia ya kunyonya maziwa ya wake zao kwa madai ya kuondoa kilevi mwilini mwao. Waache kwa sababu watawaambukiza watoto wao magonjwa kutokana na vinywa vyao kubeba bakteria," alisisitiza.

Alisema tabia hizo zinasababisha magonjwa ya kuambukiza yanayotoka kwenye kinywa cha mtu yeyote anayenyonya maziwa ya mama anayenyonyesha.

Kadhalika, alibainisha kuwa mtoto anahitaji kunyonya maziwa ya mama, hivyo kitendo cha mtu kuweka uchafu wowote kwenye maziwa hayo kinahatarisha afya yake wakati wa kunyonya.

Pia alisema ni kitendo cha aibu kwa wanaume wenye tabia hizo na jamii inatakiwa kuwaonya kwa sababu inaweza kusababisha madhara.

Aidha, alisema hali ya lishe ya watoto chini ya miaka mitano kulingana na kiashiria cha udumavu unaoonyesha kwenye Utafiti wa Hali ya Lishe (TNNS) wa mwaka 2018 kuwa asilimia 31.8 ya watoto wote nchini wana udumavu.

Alizitaja athari za udumavu kuwa ni ukuaji duni wa kimwili na kiakili na hivyo kusababisha maendeleo duni shuleni, kuongezeka kwa magonjwa na hatari kubwa ya kupata magonjwa ya kuambukiza.

Aliongeza kuwa udumavu unaathiri watoto kwa kuwa wanapokuwa watu wazima kuna uwezekano mkubwa wa kuugua magonjwa ya moyo, kisukari na saratani na kupungua kwa uwezo wa kufikiri.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Lishe kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Grace Moshi, alisema kila mwaka maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani huadhimishwa Agosti Mosi hadi 7.

Alisema mwaka huu maadhimisho hayo kitaifa yalizinduliwa mkoani Songwe yataendelea mpaka kilele chake Agosti 7, mwaka huu.

Alisema maadhimisho hayo yanaenda sambamba na kaulimbiu isemayo "Jukumu Letu Sote Kulinda Unyonyeshaji wa Maziwa ya Mama".

## TCCIA yapigia debe fursa bomba mafuta

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAFANYABIASHARA mkoani Dodoma wametakiwa kuchangamkia fursa ya ujenzi wa mradi mkubwa wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi mkoani Tanga.

Ofisa Mtendaji wa Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Dodoma, Iddi Senge, alitoa wito huo alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini hapa jana.

Senge aliwataka wafanyabiashara mkoani hapa kuchangamkia fursa ya ujenzi wa maradi huo mkubwa wa bomba la mafuta unaotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Alibainisha kuwa bomba hilo ambalo linapita kwenye baadhi ya wilaya za mkoani hapa litahitaji makandarasi na watoa huduma mbalimbali ambazo wahusika wakichangamkia zitawasaidia kukuza na kuongeza uchumi wa mkoa.

Alizitaja baadhi ya fursa ambazo wafanyabiashara wataomba kuzifanya kuwa ni usambazaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya ujenzi wa bomba hilo litakalopita wilaya za Chemba na Kondoa.

Pia alizitaja fursa zingine kuwa ni usambazaji wa vilipuzi kwa ajili upasuaji wa miamba na maji ya ujenzi wa bomba hilo kwa mkandarasi au watu wanaojenga hapo.

Senge pia alizitaja fursa zingine kuwa ni usambazaji wa mafuta kwa ajili ya magari na mitambo ya kufanyakazi ya ujenzi kwenye mradi huo.

Kutokana na uwapo wa fursa hizo, Senge aliwaalika wafanyabiasha nchini kuhudhuria mkutano mkubwa utakaowakutanisha wafanyabiashara na makandarasi na mkandarasi mkuu wa mradi huo, kampuni ya Total.

Alisema mkandarasi huyo atakutana na makundi hayo Agosti 25, mwaka huu kwenye mkutano uliondaliwa na TCCIA na Shirikla la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).



Waandishi wa habari za mitandaoni nchini wakiwa katika mafunzo ya siku tatu ya kuwajengea uwezo yaliyoandaliwa na Klabu ya Waandishi wa Habari ya Mkoa wa Arusha, jijini Dodoma jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Askofu ataka upendeleo chanjo corona

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani, ameiomba serikali kutoa kipaumbele katika utoaji chanjo ya corona kwa viongozi wa dini ili kuepuka maambukizi kutoka kwa jamii wanayoihudumia.

Dk. Chilongani alitoa ombi hilo baada ya kupoteza wachungaji 12 ambao anaamini wamepata maambukizi kutoka kwa waumini na watu wengine wanaowahudumia.

Aliayasema hayo juzi katika mkutano wa viongozi wa dini, baraza la wazee, wanasiasa wa vyama mbalimbali ulioandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka.

Akizungumza katika mkutano huo, Askofu Chilongani alisema wakiwa viongozi wa dini, wanaitwa kutoa huduma kwa wagonjwa mbalimbali na wengine wanakuwa na matatizo ya mfumo wa kupumua.

"Tunaomba serikali iliangalie hili. Watumishi wa Mungu tuko katika hali hatarishi ya kupata maambukizi ya ugonjwa wa corona," alisema Dk. Chilongani.

Kutokana na hali hiyo, alisema watumishi wa Mungu wapewe kipaumbele ili wawe salama katika utoaji huduma za kiroho katika makanisa na misikiti.

Kwa upande wake, Mtaka alisema viongozi wa dini wanapaswa kusaidia kutoa elimu kwa waumini ili kupata chanjo kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Alisema jamii imekuwa ikiamini mambo kutoka katika mitandao ya kijamii jambo ambalo sio sahihi kinachotakiwa ni kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya.

Mtaka alisema uhai wa binadamu ni mali yake mwenyewe, hivyo kila mmoja anapaswa kufuata masharti ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Hata hivyo, aliwataka viongozi wa dini kwenda kutoa elimu sahihi kwa waumini makanisani na misikitini, lakini viongozi wa siasa nao wakatoe elimu katika vikao vyao ili kusaidia jamii kutambua umuhimu wa chanjo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, aliwataka viongozi wa dini wajipange kwa ajili ya kuweka maombi ya kuombea ugonjwa huo kulingana na hali ya ugonjwa ilivyo.

Dk. Mganga alisema viongozi hatuna sababu ya kusubiri tamko la serikali kuhusu maombi kinachotakiwa ni kuomba kutokana na janga la ugonjwa huu wa corona uliopo.

Naye Askofu Dk. Eliah Mauza wa Kanisa la Endtime Harvest alisema kinachotakiwa hivi sasa ni kuendesha maombi ili kuwajengea waumini imani ya kuamini chanjo na kuombea ugonjwa wa corona ili utoweke.

Dk. Mauza alisema waumini tunapaswa kuendeleza wimbi la maombi ya kutokomeza ugonjwa huu ili uweze kuiachia dunia.



# USAID yatoa msaada kukabili TB Tanzania

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

SERIKALI ya Marekani kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imekabidhi msaada wa vifaa vya kisasa vya maabara kwa ajili ya uchunguzi wa kifua kikuu (TB) vyenye thamani ya Sh. milioni 424.36 kwenye vituo 19 vya afya katika mikoa minne ya Tanzania Bara.

Vifaa vilivyotolewa ni mashine nane za kuchunguza kifua kikuu sugu (Gene Xpert) na hadubini 11, mikoa ya Songwe, Rukwa, Katavi na Kigoma ikinufaika na msaada huo kutokana na kuwa na upungufu wa vifaa hivyo.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa jana mkoani Songwe na shirika lisilokuwa la kiserikali linalohusika na masuala ya afya la Tanzania Health Promotion Support (THPS) na vilipokewa na viongozi wa mkoa huo kwa niaba ya mikoa mingine itakayonufaika. Akikabidhi vifaa hivyo kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa THPS, Kiongozi wa Mradi wa USAID Uhuru wa Kifua Kikuu na Kupanga Uzazi, Dk. Benedicta Masanja, alisema vifaa hivyo vitasaidia kuboresha huduma za kifua kikuu.

Alisema THPS imekuwa ikifanya kazi katika mikoa hiyo minne na ilibaini upungufu wa vifaa hivyo uliokuwa unasababisha hali duni za utambuzi wa kifua kikuu kwenye jamii.

"Vifaa hivi vya utambuzi vya Gene Xpert hupunguza muda wa uchunguzi wa kifua kikuu kutoka wiki mbili hadi tatu zilizokuwa zinatumika mpaka dakika 90 hadi 120, lakini hizi hadubini zitasaidia utambuzi wa TB kwenye vituo ambavyo havitakuwa na mashine ya Gene Xpert," alisema Dk. Masanja.

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya wakuu wa mikoa yote minne, Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Cosmas Ishenye, alishukuru USAID pamoja na washirika wake kwa msaada huo kwa maelezo kuwa utasaidia kuimarisha huduma za afya katika mikoa hiyo.

Aliwataka wasimamizi wa afya katika vituo vitakavyonufaika kuhakikisha wanavitunza vizuri vifaa hivyo ili vidumu, akiwataka wataalamu kuvihifadhi kwenye eneo lenye hali nzuri ya hewa. Alisema endapo vifaa hivyo havitatunzwa vizuri, vitaharibika na lengo la wafadhili litakuwa limeharibika.

Aliwataka wananchi wa Wilaya ya Mbozi kujitokeza kwenye vituo vya afya kupima afya zao ili kubaini mapema kama wana maambukizi ya TB ili watibiwe mapema.

"Kwa niaba ya mikoa yote minne, ninakiri kuvipokea vifaa hivi vya kisasa, ninaamini kwamba vitatusaidia kuboresha huduma za afya kwa wananchi wetu, lakini ninawasihi watumishi wa afya watakaokuwa wanavitumia kuvitunza ili vilete tija," alisema Ishenye.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Nyembea Hamadi, alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa inayochangia takwimu za kifua kikuu kitaifa, akibainisha kuwa takwimu za afya za mwaka 2020 zinaonyesha watu 715 waligundulika kuugua ugonjwa huo.

Alisema mbali na kupatiwa msaada wa vifaa hivyo pia wadau hao wanawajengea uwezo watumishi wa afya katika mikoa hiyo ili waweze kuvitumia kwa usahihi katika kutambua maambukizi ya TB.

Kaimu Meneja wa Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Liberate Mleoh, alisema jukumu la kuwatambua wagonjwa wa TB na kuwaingiza kwenye matibabu ni la wizara hiyo lakini lazima ushiriki wa wadau uwapo.



Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Cosmas Ishenye (kushoto), akipokea vifaa vya kisasa vya kupima ugonjwa wa kifua kikuu juzi, vilivyotolewa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Kimataifa la Maendeleo (USAID) kutoka kwa Kiongozi wa Mradi wa USAID Uhuru wa Kifua Kikuu na Kupanga Uzazi, Dk. Benedicta Masanja (kulia), kwa ajili ya mikoa ya Songwe, Rukwa, Katavi na Kigoma. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waunga mkono kuzuia Nanenane

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WANANCHI wa Mkoa wa Mbeya wameipongeza serikali kuzuia maonyesho ya wakulima, maarufu Nanenane, mwaka huu wakidai kuwa yangechangia kuongezeka kwa maambukizi ya virusi vya corona kutokana na msongamano wa watu kwenye viwanja vya maonyesho.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi hao walisema pamoja na kwamba maonyesho hayo yana umuhimu wake kiuchumi, hali ya ugonjwa wa corona ni tishio zaidi na hivyo serikali ilifanya uamuzi sahihi.

Mmoja wa wananchi hao, Venance Mwanyela, alisema kwenye maonyesho hayo huwa wanakusanyika watu kutoka katika maeneo mbalimbali nchini na baadhi kutoka nje ya nchi na hivyo mkusanyiko huo ungekuwa hatari.

Alisema kwa sasa wanasubiri waone hali itakavyokuwa mwakani ili ikiwezekana kama ugonjwa huo utakuwa umeisha maonyesho hayo yafanyike.

"Serikali ilikuwa sahihi kuzuia maonyesho haya maana huwa kunakuwa na mkusanyiko wa watu kutoka maeneo mbalimbali wakiwamo wa kutoka mikoa ya mipakani, tusubiri tu mpaka mwakani pengine hali itakuwa imetengamaa," alisema Mwanjela.

Denis Mwandobo, Mkazi wa Ilemi jijini Mbeya, alisema hata serikali ingeruhusu na kutoa maagizo ya kuchukua tahadhari, bado kungekuwa na tatizo kwa kuwa baadhi ya watu huwa ni wakaidi wa kutii maelekezo.

Alisema ugonjwa wa corona ni hatari zaidi kuliko hasara ambayo imepatikana kutokana na kuahirishwa kwa maonyesho hayo kwa mwaka huu.

Februari 10 mwaka huu, Waziri wa Kilimo, Profesa Adolph Mkenda, alitangaza kusitishwa kwa maonyesho ya wakulima huku akielekeza fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya maandalizi hayo, zitumike kuandaa mashamba darasa kwenye vijiji kwa ajili ya kufundishia wakulima.

# Mbunge aishukuru serikali kwa mradi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, ameishukuru serikali kwa kukamilisha mradi wa maji wa Shongo uliogharimu Sh. bilioni 3.3 na kusaidia kutatua kero ya muda mrefu ya maji katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Njeza alitoa shukrani hizo wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilipofanya ziara ya kukagua mradi huo ambao umejengwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MbeyaWSSA) kwa kutumia mapato yake ya ndani.

Mradi huo ulianza kujengwa mwaka 2019 ikiwa ni utekelezaji wa agizo la aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, alipokuwa ziarani mkoani Mbeya baada ya wananchi wa mji huo kulalamikia kero hiyo.

Akizungumza wakati wa kukagua mradi huo, Njeza alisema tatizo la ukosefu wa maji katika Mji wa Mbalizi ni miongoni mwa vitu vilivyokuwa vinamnyima usingizi kutokana na kero ambayo wananchi wa mji huo walikuwa wanalalamika kila siku.

Mbunge huyo alikumbusha kuwa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka jana, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika wilaya hiyo na yeye mwenyewe waliwaahidi wananchi kuwa kero hiyo itakuwa historia, lakini alikuwa na wasiwasi na utekelezaji wake.

"Mradi huu ni mkubwa na ni wa kisasa sana, mbali na kusaidia wananchi wa Mji wa Mbalizi pia unasaidia wananchi wengine wa Bonde la Songwe na Kijiji cha Ilota ambacho tulikiombea na tumepewa Sh. milioni 200 kwa ajili ya kupeleka maji," alisema Njeza.

Alisema mradi huo umekuwa wa mfano katika jimbo hilo huku akiwataka watendaji wanapotekeleza miradi mingine, watumie mbinu iliyotumika kwenye mradi huo ambao umetekelezwa ndani ya muda mfupi na kwa kutumia mafundi wa ndani.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Mbeya, Hakim Mwalupindi, alisema pamoja na kwamba mradi huo umekamilika, mamlaka ya maji inatakiwa kubadilisha baadhi ya mabomba ya zamani ili kupunguza upotevu wa maji.

Alisema mradi huo una maji mengi lakini mabomba hayo ya zamani yanashindwa kuhimili kasi ya maji na hivyo kupasuka mara kwa mara, hali ambayo inasababisha upotevu wa maji.

"Sisi kama wasimamizi wa serikali tumefurahishwa sana na utekelezaji wa mradi huu maana umejengwa kwa viwango, kama ni duka basi mnauza vizuri ndiyo maana kiongozi yeyote akija lazima tumlete hapa ili auangalie," alisema Mwalupindi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka wananchi wa Mji wa Mbalizi kuendelea kulipia ankara zao ili uendeshaji wa mradi huo uwe endelevu ikiwamo kurekebisha baadhi ya maeneo ambayo yatakuwa yanaharibika.

Homera alisema mradi huo ni miongoni mwa miradi muhimu katika Mkoa wa Mbeya na hivyo akawataka wananchi kuendelea kuilinda miundombinu ili idumu.



# Jumuiya ya JUMAZA yakimbilia Mahakama Kuu kesi ya vileo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAHAKAMA Kuu Zanzibar imeanza kusikiliza kesi ya Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Bodi ya Udhibiti wa vileo Zanzibar baada ya kesi ya awali kufutwa na Jaji Rabia Hussein Muhammed kwa madai ya kufunguliwa kinyume na sheria.

Katika kesi ya awali Jaji Rabia alisema JUMAZA walipaswa kufungua kesi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Mapinduzi ya Zanzibar badala ya Bodi ya Udhibiti wa Vileo baada ya kutoa indhari ya siku 60 jambo ambalo halikufanyika.

kesi hiyo imetajwa kwa mara ya kwanza jana mbele ya Jaji wa Mahakama kuu Abdulhakim Ameri Issa, upande wa serikali unawakilishwa na mwanasheria kutoka ofisi ya Mwanasheria Mkuu na JUMAZA wanawakilishwa na Wakili Omar Shekhe Omar.

Kwa mujibu wa hati ya kiapo ya waombewa inadai Bodi ya Vileo Zanzibar imetoa vibali kwa kampuni za kuingiza pombe Zanzibar zaidi ya kampuni tatu kinyume na kifungu cha 33(1) ya Sheria ya Vileo Namba 9 ya mwaka 2020 pamoja na kushindwa kusimamia sheria ya baa na maduka ya pombe kuwa umbali wa mita 1,000 kutoka katika maeneo ya huduma za jamii kama shule, nyumba za ibada, hospitali na makazi.

"Nawakilisha waombewa katika shauri hili namba moja na mbili... tunaomba kupewa muda wa kujibu hati ya kiapo dhidi ya shauri hili," alisema Mwanasheria wa Serikali kutoka kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Habiba Haji Ali.

Upande wa Wakili Omar Shekha Omar, alisema hawana pingamizi na Mahakama kutoa muda, kwa upande wa serikali kupewa muda wa kujibu hati ya kiapo dhidi ya kesi iliyofunguliwa mwaka huu.

"Sina pingamizi kwa upande wa wadaiwa kupewa muda wa kujibu hati ya kiapo na mahakama yako," alisema Wakili Omar.

Alisema wameamua kufungua tena kesi hiyo baada ya wateja wake kutoridhishwa na uamuzi uliotolewa na Jaji Rabia baada ya kuitupilia mbali kesi hiyo Juni, mwaka huu.

Kwa upande wake Jaji Abdulhakim alisema anatoa muda wa wiki mbili, upande wa serikali kuwasilisha majibu ya hati ya kiapo ya maombi ya walalamikiwa hadi Agosti 19 kabla ya kesi kutajwa Septemba 13, mwaka huu.

Naye Katibu wa Kamati ya Maadili na Baraza la Taasisi za Kiislamu, Shehe Abdallah Mnubi Abasi, alisema wameamua kuirejesha tena mahakamani kesi hiyo baada ya kutoridhishwa na uamuzi wa awali wa Jaji Rabia katika kesi namba tatu dhidi ya Bodi ya Vileo baada ya kuitupilia mbali kwa madai ya kufunguliwa kinyume na sheria.

Kesi hiyo imeibua mjadala mkubwa katika jamii baada ya kuanza kutekelezwa kwa sheria mpya ya udhibiti wa vileo namba tisa ya mwaka 2020 iliyoanza kutumika baada ya kusainiwa na aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, Mei 11, mwaka 2020.

## Zanzibar, Msumbiji kuendeleza ushirikiano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendeleza ushirikiano na uhusiano wake na Msumbiji katika azima ya kuwajengea mustakabali mzuri wananchi wa pande zote mbili.

Hemed alieleza hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi mdogo wa Msumbiji aliyepo mjini hapa.

Alisema, kuna kila sababu ya kuendeleza uhusiano kati ya Zanzibar na Msumbiji uliodumu kwa muda mrefu sasa kutokana na mwingiliano wa watu unaosababishwa na harakati mbalimbali za kimaisha ikiwamo biashara.

Makamu wa Pili wa Rais alisema, wapo Wazanzibar wengi wanaoendesha maisha yao nchini Msumbiji kutokana na ushirikiano mwema uliojengwa miaka mingi iliyopita.

Hemed alimweleza Balozi huyo kuwa Zanzibar kuna fursa nyingi zinazopatikana akitoa mfano sekta ya utalii na bidhaa zitokanazo na masuala ya viungo (Spices).

Naye Balozi Mdogo wa Msumbiji anayefanya kazi zake Zanzibar, Agostino Abacar Trinta, alisema kwamba nchi yake itaendelea kushirikiana na kufanya kazi zake kwa karibu na Serikali ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa lengo la kuimarisha diplomasia.



Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka Zanzibar, Issa Haji Gavu, akipiga chanjo ya corona katika kituo cha chanjo cha Hospitali ya Aga Khan, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mfumko wa bei wapaa visiwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KASI ya mfumko wa bei imefikia asilimia 2.2 kwa mwaka ulioishia Julai 2021 kutoka asilimia 1.9 mwezi Juni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.3.

Mkuu wa Kitengo cha Takwimu za bei Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Khamis Abdulrahman Msham, alisema hayo alipokuwa akiwasilisha ripoti ya mfumko kwa mwezi Julai huko Mazizini mjini Unguja.

Alisema, kiwango cha mfumko wa bei za chakula na vinywaji visivyokuwa na vileo imeongezeka na kufikia asilimia 1.2 mwezi Julai, kutoka asilimia 0.1 mwezi Juni.

Alisema, faharisi za bei ziliongezeka na kufikia asilimia 117.3 mnamo Julai 2021 ikilinganishwa na 114.8 zilizorekodiwa Julai 2020.

Alizitaja bidhaa zilizochangia kuongezeka kwa mfumko wa bei wa mwaka na asilimia kwenye mabano kuwa ni mchele aina ya mapembe (4.7), Jasmin (5.2), unga wa ngano (10.0), ndizi za mtwike (23.7), samaki (9.5) mafuta ya kula ya OKI (18.9), petroli (32.9) na dizeli (19.7).

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Takwimu za Kiuchumi Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Abdulrauf Ramadhan, alisema, pamoja na kupanda kidogo kwa mfumuko, hali ya uchumi imeendelea kubaki vizuri huku kukiwa na bidhaa za kutosha kwenye masoko na uzalishaji mzuri.

Alisema, kuwapo kwenye tarakimu moja ni njia bora ya kuwavutia wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza nchini kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Mchumi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Ulrick Mbumbuvi, alisema, kuendelea kuongezeka kwa mfumko kumechangiwa na bidhaa za kimataifa yakiwamo mafuta huku kwenye masoko na uzalishaji yakiwa vizuri.

Mhadhiri wa Uchumi Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Dk. Stella Ngoma Hassan, alisema bado hali inaonyesha kuwa vizuri kiuchumi na kuleta faraja kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

IPO PUGU KAJIUNGENI, ZIPO MBILI. MOJA HAIJAMALIZIKA, FREMU SITA ZA BIASHARA INA OFFER. BEI NI MIL. 65.

KWA MAWASILIANO:

0787 – 608011 / 0762 944949.

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 34 YA MWAKA 2021**
**APOLINARY ALOYCE ……………………….MDAI**
**DHIDI YA**
**RAMADHANI IDRISSA KIMARO ………………………….. MDAIWA**
**KWA: RAMADHANI IDRISSA KIMARO**

**POPOTE ULIPO**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba Mdai amefungua madai dhidi yako nakala yake inapatikana katika mahakama hii.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo **tarehe 19/08/2021 saa 2:30 Asubuh**i na unatakiwa kuwepo au kuwakilishwa Kisheria Pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya madai haya
Zingatia kwamba kutokufika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kuwepo, na maamuzi kutolewa.
Imetolewa leo hii Mbele yangu na Mhuri wa **Mahakama tarehe 03/08/2021**

**HAKIMU MKAZI**
**MWANZA**

116394502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANI**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 69/ 2019**
**(Asilia Shauri la Jinai Na.2/2018,Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**
**JAMHURI…………………………………MRUFANI**
**DHIDI YA**
**JOSEPH JUMA KYANDO……………MJIBU RUFAA**
**KWA BWANA : JOSEPH JUMA KYANDO**
**POPOTE ULIPO…......TANZANIA.**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya **Tarehe 27/08/2021** siku ya Ijumaa **saa 03.00 asubuhi** bila kukosa.
**ELEWA KWAMBA,**Ukikosa kufika siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila **WEWE** kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii **Tarehe 13 Mwezi July, 2021.**

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

116394902

---

**MBEYA**
**KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 77 2019**
**(Asili Shauri la Hujuma Na.1/2018.Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**

**JAMHURI……………………………MRUFANI**
**DHIDI YA**
**KENEDY LUPEMBE SIMSOKWE…MJIBURUFAA NA.1**
**MATHEW ELIKANA MWANJAL….MJIBU RUFAA NA.2**
**SHABAN MKWICHE…………..........MJIBU RUFAA NA.3**
**KWA BWANA: 1.KENEDY LUPEMBE SIMSOKWE**
**2.MATHEW ELIKANA MWANJALA**
**3.SHABAN MKWICHE**

**POPOTE MLIPO-TANZANIA.**
**KUITWA SHAURINI**

**Mnaarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya Tarehe 27/09/2021 siku ya Jumanne saa 03.00 asubuhi bila kukosa, ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.**
**ELEWENI KWAMBA,Ukikosa kufika siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila WEWE kuwepo na Uamuzi kutolewa.**
**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leoTarehe 09 .07. 2021.**

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

116395002

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**HENRICK E. DASTAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4645/0015** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MWANZA ALLIANCE SEKONDARI mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/381935/2021.**

116393102

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISDTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**LAND APPEAL 26 OF 2020**
**Originated from land case 255 of 2017**
**District Land and Housing Tribunal of Arusha at Arusha**
**KAREN YOHANES…………………APPELLANT**
**VERSUS**
**EZEKIEL JOSEPH & ANOTHER ….RESPONDENT**
**NOTICE OF HEARING**
**TO :**
**EZEKIEL JOSEPH**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High court at Arusha on **24th day of AUGUST, 2021 at 09:00 am in the forenoon.**
**YOU** may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for hearing, the court may proceed in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of the **COURT** this 4th day of August,2021

**M.MAHUMBUGA**
**DEPUTY REGISTRAR ARUSHA.**

116395502

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Waziri ampa mtihani bosi mpya TANROADS

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, ametoa maagizo sita kwa Mtendaji Mkuu mpya wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Rogatus Mativila.

Miongoni mwa maagizo hayo ni kuhakikisha ujenzi wa madaraja pamoja na barabara zinapitika nyakati zote.

Mengine ni usimamizi wa mizani kuhakikisha anadhibiti uzito wa magari, ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi unaosababishwa na kuchelewa kwa misamaha ya kodi, Mameneja kukaimu nafasi kwa muda mrefu, ucheleweshaji wa malipo ya fidia na utekelezaji wa miradi kwa uadilifu, weledi na kwa wakati.

Alitoa maagizo hayo jana, jijini Dar es Salaam wakati wa kumkabidhi ofisi Mtendaji Mkuu huyo, akimtaka kuhakikisha anasimamia vyema mtandao wa barabara nchini wenye urefu wa kilometa 36,000.

"Kazi hii ni kubwa, inahitaji kujitolea na ushirikiano kutoka kwa wadau wote wa sekta hii. Niwaombe ndugu zangu wa TANROADS, mpeni ushirikiano mtendaji mkuu kama ilivyokuwa siku zote kwani imejijengea heshima kubwa nchi kwa kufanya kazi kwa weledi," aliagiza.

Mbali na hayo, Dk. Chamuriho aliwataka watendaji wa TANROADS kuhakikisha wanapunguza malalamiko mbalimbali ikiwamo ucheleweshaji wa miradi inayosababishwa na kuchelewa kwa misamaha ya kodi na ujenzi wa barabara chini ya kiwango.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mativila alimhakikishia Waziri Chamuriho kufanya kazi kwa ushirikiano kwa kuwa amekuwa katika sekta hiyo kwa muda mrefu, hivyo anazifahamu kero zote zilizopo na aliahidi kujifunza utamaduni wa utendaji kazi kwa haraka na kwa weledi.

Alisema wakati wa uongozi wake, atatumia vyema miongozo waliyokabidhiwa na serikali pamoja na elimu waliyonayo na weledi katika kuhakikisha majukumu yote yanatekelezwa kwa umakini pamoja na kutatua shida zote kwa wakati.

"Niwatake watumishi wenzangu kujitathimini na kutokusubiri kutathimiwa pamoja na kuepuka kufanya kazi kwa mazoea, ili kuendeleza taasisi hii muhimu nchini katika kukuza uchumi wa taifa," alisema.

Makabidhiano hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali akiwamo Katibu Mkuu Sekta ya Ujenzi, Joseph Malongo, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Raphael Nombo, Bodi ya TANROADS na Manejimenti ya TANROADS.

# Madeni ya Posta kutua kwa Samia

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, ameagiza andiko la madeni sugu ya Shirika la Posta Tanzania likamilike haraka, ili liwasilishwe kwenye Baraza la Mawaziri.

Dk. Ndugulile aliagiza hayo, jana jijini Dar es Salaam, alipofungua kikao maalum cha siku tano cha Shirika la Posta kilichowakutanisha watendaji wake wa mikoa mbalimbali, ili kutathmini safari ya mwaka uliopita na malengo mapya ya mwaka mpya.

Kikao hicho kilihusisha Mameneja Wakuu, Wakuu wa Idara na Vitengo Makao Makuu, Mameneja wa Mikoa Tanzania Bara na Zanzibar na viongozi wa vyama vya wafanyakazi.

"Yapo madeni sugu yaliyopo Posta ninahitaji kuliona hilo andiko, ili lipelekwe kwenye Baraza la Mawaziri nilishawaambia muda mrefu, ninataka ndani ya muda mfupi likamilike, ninataka katika mwaka huu tumalizane, ili tuwe na shirika linalofanya kazi na lenye afya," alisema.

Pia, alilitaka shirika limalize migogoro na mgawanyo wa mali kati yake na Kampuni ya Simu ya Tanzania (TTCL), ambazo awali ziliungana na baadaye kugawanywa.

"Sitegemei wala sitaraji katika kikao cha robo mwaka kinachokuja Septemba niambiwe bado kuna migogoro. Kikao kijacho Kaimu Posta Masta na Mkurugenzi Mkuu TTCL mje mnipe taarifa ya mali, majengo mmefikia hatua gani na mali zitangazwe kwenye Gazeti la Serikali," aliagiza.

Kuhusu mameneja wa mikoa na viongozi wengine waliokutana siku hiyo, waziri huyo aliwataka wapunguze matumizi yasiyo ya lazima katika maeneo yao na wahakikishe mikoa yao inazalisha fedha za kujiendesha na atakayeshindwa ajue hastahili. Vilevile, alielekeza kila baada ya miezi mitatu, watendaji wakuu wakutane na wamweleze malengo, mafanikio na matatizo yanayowakabili.

Alisema katika kuhakikisha shirika linaendelea kufanya vizuri na kuwa la ushindani kimataifa, watendaji wake wanapaswa kujenga tabia ya kujifunza kwa waliopita, ili kupata uzoefu.

"Sitegemei magenge ndani ya shirika, kazi ikiwa nzuri tutakuona tu. Wizara itaendelea kuwaunga mkono, ili muende vizuri zaidi, zipo hatua tunaendelea kuchukua mchakato wa kuhakikisha tunapata zile fedha kutoka Hazina.

"Naibu Katibu Mkuu fuatilia zitoke kwa wakati, nielekeze fedha hizi mkizipata sio kulipa madeni, bali kuleta mabadiliko chanya," alisema.

Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Macrice Mbodo, alisema kwa siku tano washiriki watapewa mafunzo mbalimbali ikiwamo kujengwa uelewa wa kusimamia rasilimali za shirika na kupata uzoefu kupitia taasisi zilizofanikiwa.

"Watafundishwa ustaarabu na itifaki, usalama na utunzani wa siri, uelewa wa kutumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)," alisema. Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Posta Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Haruni Lemanya, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wake, alisema ni vizuri wajue sera ya ubora ya shirika, ili liende kisasa.

Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba, alilikumbusha Shirika la Posta kuwa kujenga hadhi ya shirika ni mchakato unaoendelea, lakini kulibomoa ni rahisi, hivyo wahakikishe wanamsaidia Kaimu Postamasta kulilinda wakati wote.

***Imeandaliwa Romana Mallya na Mary Geofrey**




Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba (kushoto), akimpongeza Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi, baada ya uzinduzi wa huduma ya TCB Internet Banking, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya TCB yazindua malipo kwa mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) imekuwa benki ya kwanza nchini kuunganisha huduma zake za kibenki mtandaoni na mifumo yote ya kitaifa ya malipo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Sabasaba Moshingi, amesema maboresho yaliyofanyiwa mfumo wa suluhisho hilo ya kidijitali unaifanya huduma ya TCB Internet Banking kuwa ya kipekee na isiyokuwa na mpinzani sokoni.

"Suluhisho hili limebuniwa na kutengenezwa na wataalamu wetu wenyewe bila gharama yoyote na ubora wake dhidi ya mifumo mingine ni kuunganishwa kwake na mifumo yote ya kitaifa ya malipo," Moshingi alibainisha jana wakati wa unzinduzi wake, jijini Dar es Salaam.

"Tungeinunua sokoni ingetugharimu kati ya Dola 300,000 na 500,000," alifafanua akionyesha unafuu wake kwa kuwa bei hizo ni sawa na Sh. milioni 695.7 na karibu Sh. bilioni 1.16, mtawalia.

Kwa mujibu wa Moshingi, uwekezaji wa kuboresha huduma hiyo ni sehemu ya mpango mkakati wa kuimarisha suhuhishi za kibenki za TCB na kuzifanya za kisasa zaidi, ili ziendane na mahitaji ya soko.

Alisema maboresho ya TCB Internet Banking, pia yanalenga kuiwezesha benki hiyo kujipanga vizuri zaidi kibiashara na kujiimarisha kiushindani sokoni.

Serikali imeipongeza benki hiyo kwa kufanya maboresho hayo na kusema yataongeza thamani kwenye mifumo ya kitaifa ya malipo.

Akizumgumza kabla ya kuizindua rasmi huduma hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema uwekezaji huo pia unalipa na kuifanya TCB kuwa 'tishio'.

Kiongozi huyo amewataka wananchi na taasisi zote kujiunga na mfumo huo mpya wa TCB, ili wafanye miamala ya kifedha kwa urahisi, usalama na uharaka, hivyo kuongeza ufanisi katika shughuli zao.

"Nimefurahi kusikia kuwa mfumo huu pia umeunganishwa moja kwa moja na mfumo wa MUSE, ili kurahisisha taasisi za serikali kufanya malipo pasipo na ulazima wa kutembelea benki," Tutuba alisema.


MUSE ni mfumo wa ulipaji serikalini, ambao ni sehemu ya mchakato wa serikali mtandao kwa ajili ya kuziwezesha taasisi za umma na makundi mengine kama watumishi, raia, wanafunzi na wafanyabiashara kupata taarifa na huduma kwa njia ya intaneti.

Katibu Mkuu Tutuba aliitaka TCB kutumia umahiri wake wa ubunifu kusaidia kutafuta ufumbuzi wa masuala mbalimbali na kusaidia kutatua vikwazo vingine.

Akiutambulisha mfumo huo, Meneja Mkuu Suluhishi za Biashara wa TCB, Leonard Katamba, alisema huduma hiyo imebuniwa kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na maendeleo ya kidijitali ya siku za usoni.

"Huduma ya TCB Internet Banking itatoa wigo mpana wa huduma za kibenki kwa wateja wetu; taasisi za serikali kampuni, mashirika ya dini na mengine yasiyo ya kiserikali, wafanyabiashara wakubwa na wadogo, wafanyakazi, vikundi mbalimbali, taasisi za elimu pamoja na mtu mmoja mmoja," alisema.

# Ings atua Aston Villa




**LONDON,** England

ASTON Villa imefanya usajili wa kushtukiza kwa kumsajili straika Danny Ings kutoka Southampton.

Ings mwenye umri wa miaka 29, alifunga mabao 14 msimu uliopita kwa nchi na klabu yake na amesaini mkataba wa miaka mitatu na ada yake imeripotiwa kuwa pauni milioni 30.

Huku Jack Grealish akiondoka Villa na kujiunga na Manchester City, wakaamua kumchukua Ings na kocha, Dean Smith akasifia usajili huo.


"Danny ni mchezaji wa kiwango cha juu kwenye Ligi Kuu England ambaye amefunga mabao popote anapocheza," alisema Smith.

"Yeye ni mchezaji wa kiwango cha juu na nina imani atakuwa msaada mkubwa kwenye kikosi chetu.

"Nina furaha kumkaribisha Danny kwenye klabu kubwa kama hii, naamini atakuwa sehemu bora zaidi hapa."

Ings ambaye alibakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake, katika maisha yake pale Southampton alifunga mabao 46 katika mechi 100 baada ya kutua hapo akitokea Liverpool mwaka 2018.

# Alisson ajifunga upya Liverpool



**LIVERPOOL,** England

ALISSON amekuwa mchezaji wa hivi karibuni kujifunga hapo Liverpool kwa kusaini mkataba na miamba hiyo ya dimba la Anfield.

'Wekundu' hao walitangaza "mkataba wa muda mrefu" kwa golikipa wake huyo Jumatano, na sasa atakaa hapo hadi Juni mwaka 2027.

Alisson ameungana na Trent Alexander-Arnold na Fabinho kuongeza mkataba mpya kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu England.

"Nafikiri sikupoteza muda mwingine kwa kuwaza kuhusu hili," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil akiiambia tovuti rasmi ya Liverpool.

"Ni kitu fulani ambacho tumekijenga kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kujiamini, naiamini klabu na klabu ipo moyoni mwangu.

"Mimi na familia yangu, tuna furaha kubwa hapa. Watoto wangu wakifurahia maisha hapa England.

"Furaha yangu ni kuendelea kukaa hapa na kufanya kazi kwa uwezo wangu na ninaamini nitakuwa na wakati bora hapa."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alijiunga na Liverpool kutoka AS Roma mwaka 2018 na alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya katika msimu wake wa kwanza nchini England.

# Kane kukosa mechi ya kwanza EPL




**LONDON,** England

HARRY Kane hataichezea Tottenham Hotspur kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu England dhidi ya Manchester City.

Hiyo ni kwa sababu atakuwa bado amejitenga baada ya kutoka likizo kabla ya kujiunga na mazoezi ya kikosi hicho.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, aliiongoza England kufika fainali ya Euro 2020, ambapo walifungwa na Italia kwa changamoto ya mikwaju ya penalti.

Tangu hapo hakuweza kurudi mazoezini, huku kukiwa na uvumi kwamba analazimisha kuhama kwenda Manchester City.

Gazeti la Telegraph limeripoti kwamba, Kane alienda likizo kule Florida Marekani na Bahamas, na hiyo maana yake hajacheza mchezo wowote wa maandalizi ya msimu na Spurs kabla ya kuivaa City Agosti 15.

City wataendelea na mpango wao wa kutaka kumsajili Kane baada ya kukamilisha uhamisho wa Jack Grealish kutoka Aston Villa, ingawa Tottenham na Mwenyekiti Daniel Levy bado wanaamini mchezaji huyo hataondoka kipindi hiki cha majira ya joto.

## HABARI MICHEZO



# Eriksen atua mazoezi Inter

**MILAN,** Italia

CHRISTIAN Eriksen amerudi uwanja wa mazoezi ya Inter Milan kwa mara ya kwanza tangu alipokumbwa na shambulizi la moyo kwenye michuano ya Euro 2020 katika mchezo wa ufunguzi wa Denmark dhidi ya Finland.

Tukio hilo lilitokea Juni, wakati Eriksen alipodondoka na kuzimia uwanjani, huku wachezaji wenzake wakiweka uzio wa kumlinda ili asipigwe picha.

Alikimbizwa hospitali na kufanyiwa operesheni ya moyo ambayo ilifanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Eriksen mwenye umri wa miaka 29, aliwekewa 'pacemaker' (betri kwenye moyo) na baadaye alirudi Denmark, ambako alipata matibabu mengine zaidi na sasa amepona.

Kiungo huyo wa zamani wa Tottenham, aliwasili kwenye viwanja vya mazoezi vya Inter Jumatano na mshindi huyo wa taji la Serie A 2020-21, alisema anajisikia "hali nzuri kiafya."

Taarifa ya klabu hiyo ilisema: "Eriksen, ambaye alikuja kuwasabahi makocha, wachezaji wenzake na maofisa wote wa timu, hali yake ni nzuri na yupo salama kabisa.

"Eriksen ataendelea kufuatilia programu ya matibabu chini ya madaktari wa Denmark jijini Copenhagen, ambapo wataendeatimu ya madaktari wa Inter Milan watakuwa wakipewa taarifa kila wakati."

Hata hivyo, uwezekano wa Eriksen kurudi uwanjani kucheza ni mdogo sana, kwa sababu sheria za nchini Italia, haziruhusu mchezaji kucheza akiwa na mashine kwenye moyo wake.

# Van Gaal akabidhiwa mikoba ya Uholanzi

**AMSTERDAM,** Uholanzi



SHIRIKISHO la Soka la Uholanzi limemteua tena Louis van Gaal kuwa Kocha Mkuu wa timu ya Taifa hilo kwa mkataba wa mwaka mmoja ambao utafikia kikomo mwaka 2022.

Van Gaal anachukua jukumu la kukiongoza kikosi cha Uholanzi kwa mara ya tatu, ambapo awali alikuwa akikiongoza kuanzia mwaka 2000 hadi 2001 na kisha mwaka 2012 hadi 2014.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 69, atasimamia jukumu la kuhakikisha kikosi cha Uholanzi kinafuzu Fainali za Kombe la Dunia la 2022, na mkataba wake utaendelea hadi mwisho wa Fainali hizo zitakazonguruma nchini Qatar kwa mara ya kwanza.

Van Gaal aliwahi kustaafu shughuli za ukocha, kwa kigezo cha kupata msukumo kutoka kwenye familia yake, lakini kurejea tena kazini kunadhihirisha bado anaipenda kazi hiyo ambayo ameifanya akiwa kama mchezaji na kisha mkuu wa benchi la ufundi.

Maamuzi ya Shirikisho la Soka nchini Uholanzi ya kumkabidhi kikosi kocha huyo wa zamani wa klabu za Manchester United, FC Bayern Munich na Ajax Amsterdam, yametokana na kuondoka kwa Frank de Boer.

De Boer, aliachana na Uholanzi, baada ya 'The Orange' hao kushindwa kufurukuta kwenye Fainali za EURO 2020 zilizomalizika Julai jijini London kwa Italia kuwa mabingwa.

Uholanzi iliondolewa kwenye Fainali za Euro 2020 katika hatua ya mtoano wa 16-Bora.

# Lingard hataki kuondoka United

**MANCHESTER,** England




BAADA ya kuwa na wakati mzuri kule West Ham United, Jesse Lingard, alirejea kwa kishindo Manchester United na ameweka wazi, hana mpango wa kuondoka Old Trafford.

Jesse alikuwa akisugua benchi kwa muda mrefu ndani ya kikosi cha kocha Ole Gunnar Solskjaer kabla ya kujiunga na 'Wagonga Nyundo' hao kwa mkopo wa miezi sita msimu uliopita.

Akiwa Uwanja wa London, Lingard alionyesha ubora wake kwa kupachika mabao tisa katika michezo 16 ikiwa ni sambamba na kuitumikia England kwenye michezo ya kujiandaa na Euro 2020.

Lingard akarejea United kuendelea alipoishia msimu uliopita, safari hii, mchezaji huyu, si yule aliyeondoka kwa mkopo.

Imeripotiwa kuwa Lingard ameweka wazi lengo lake la kutaka kubaki United na kuipambania namba kwenye kikosi cha kwanza chini ya Solskjaer.

West Ham walikuwa na shauku kubwa ya kutaka kumsajili moja kwa moja lakini kwa hali ilivyo kwa sasa, timu hiyo imekiri kuwa na uwezekano wa asilimia 10 tu za kuweza kumsajili kutokana na uwezo anaoendelea kuuonyesha United.

## KWA UFUPI

### CHELSEA KURUDI KWA LUKAKU

INTER Milan inatarajia Chelsea kurejea na dau bora lenye thamani ya pauni milioni 110, kwa ajili ya mshambuliaji raia wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, baada ya kukataa ofa yao ya awali ya pauni milioni 85 pamoja na mlinzi Mhispania Marcos Alonso, 30. (**Mail**)

### VILLA KUMSAJILI CANTWELL

ASTON Villa wanatarajia kufuatilia mkataba na kiungo wa kati wa Norwich, Todd Cantwell mwenye umri wa miaka 23, baada ya Jack Grealish kukamilisha uhamisho wake wa pauni milioni 100 kuelekea Uwanja wa Etihad. (**Sky Sports**)

### ABRAHAM ATAKIWA ATALANTA

ATALANTA watafanya mazungumzo na Chelsea wikendi hii kujadili uwezekano wa mkataba kwa ajili ya mshambuliaji wa England, Tammy Abraham, 23. (**Gianluca di Marzo**)

### POGBA KUAMUA UNITED

PAUL Pogba ataanza msimu na Manchester United, lakini atafanya uamuzi kuhusu hali yake ya baadaye kabla ya muda wa mwisho wa kipindi cha uhamisho, huku PSG ikiwa bado inamtaka kiungo huyo wa kati Mfaransa mwenye umri wa miaka 28. (**Telegraph**)

### MADUEKE ATAKIWA SPURS

TOTTENHAM Hotspur inataka kusaini mkataba na mshambuliaji wa kati msimu huu anayechezea klabu ya PSV Eindhoven, Noni Madueke mwenye umri wa miaka 21. (**Standard**)

### COUTINHO AWANIWA SPURS

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 28, ni miongoni mwa wachezaji ambao Tottenham Hotspur italenga kuwachukua iwapo watamuuza mshambuliaji wao, Harry Kane, 28. (**Mundo Deportivo**)

### MESSI KUJIFUNGA UPYA

LIONEL Messi anatarajiwa kusaini mkataba mpya na Barcelona baadaye wiki hii. Mkataba wa awali ulimalizika mwezi uliopita, lakini mshambuliaji huyo wa Argentina amekubali kwa maneno mkataba mwingine wa miaka mitano ambapo malipo yake yatapunguzwa kwa asilimia 50. (**Sky Sports**)

### LEICESTER YAIGOMEA ARSENAL

LEICESTER City wamekataa dau la mchezaji pamoja na fedha kutoka Arsenal kwa ajili ya kiungo wa kati wa England, James Maddison mwenye umri wa miaka 24. (**Football Insider**)

### CHELSEA YAKWAMA KWA KOUNDE

JARIBIO la Chelsea la kumsajili mlinzi wa Sevilla, Jules Kounde limekwama kwa sababu Mfaransa mwenzake, Kurt Zouma, 26, ambaye walitumaini kuwa wangemuuza ili kutoa nafasi kwa ajili ya kijana huyo mwenye umri wa miaka 22, kukataa. (**Guardian**)

### SKIPP ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE wameeleza nia yao ya kutaka kumsajili Oliver Skipp mwenye umri wa miaka 20, kutoka kikosi cha England cha vijana wenye umri chini ya miaka 21, kutoka Tottenham. (**Mail**)

### DAVIES KUTUA SHEFFIELD

KLABU ya Sheffield United ina matumaini ya kumsajili Ben Davies kwa mkopo kutoka klabu ya Liverpool. Mlinzi huyo Muingereza mwenye umri wa miaka 25, amecheza mara moja tu tangu aliposaini mkataba Preston Januari.(**Goal**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GREALISH AWEKA REKODI MPYA AKITUA MAN CITY

●●● Ni baada ya kukubali kuondoka Aston Villa na kujiunga na miamba hiyo ya Etihad kwa...

**MANCHESTER,** England

JACK Grealish ataweka historia ya kuwa mchezaji wa kwanza Muingereza kulipiwa ada ya uhamisho kiasi cha pauni milioni 100, baada ya kukubali kuondoka Aston Villa, kwenda Manchester City.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, jana alitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya kabla ya kujiunga rasmi na Man City ndani ya saa 24 zijazo na kusaini mkataba wa miaka mitano.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England wamevunja rekodi ya uhamisho kwenye soka la Uingereza, baada ya wiki iliyopita kuthibitisha kwamba wamekubali kufikia ada inayotakiwa kuipata huduma ya Grealish.

**Mwandishi wa Sportsmail, Chris Wheeler, Machi mwaka huu aliripoti kwamba, City wana nafasi kubwa ya kumsajili Grealish kipindi hiki cha majira ya joto.**

Matt Hughes, alibainisha Mei mwaka huu kwamba, City watakuwa tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 100, kwa ajili ya kumsajili Grealish.

Na Juni, Daily Mail ikaripoti kuwa City wapo tayari kutoa pauni milioni 100 kwa ajili ya kumsajili Grealish, licha ya Villa kumpa ofa ya mkataba mpya.

Na kama kiungo huyo wa kimataifa wa England atakamilisha dili hilo ndani ya wakati, ana nafasi ya kuichezea Man City kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Leicester City kesho, Jumamosi.

Grealish sasa amevunja rekodi ya pauni milioni 89, ambayo ilitolewa na Manchester United wakati walipomsajili tena kiungo wa Ufaransa, Paul Pogba akitokea Juventus mwaka 2016.

Nyota huyo alirejea kwenye kikosi cha Aston Villa mara baada ya kumalizika likizo baada ya michuano ya Euro 2020 akiwa na England.

Villa walikuwa kwenye mpango wa kumpa ofa mpya Grealish, ambapo walipanga kumpa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki.

## HABARI MICHEZO

# WAKIMBIAJI KIMATAIFA WAFURIKA USAJILI CRDB BANK MARATHON

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI zikiwa zimebaki siku 10 kuelekea CRDB Bank Marathon, wakimbiaji wa kimataifa kutoka nje ya Tanzania zaidi ya 700, tayari wamejisajili kushiriki mbio hizo zinazotegemewa kujumuisha wakimbiaji 5,000, imeelezwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, wakati akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam jana, mwitikio huo wa wakimbiaji wa kimataifa unatokana na kuvutiwa na lengo la mbio hizo kusaidia jamii pamoja na kusajiliwa kimataifa na Chama cha Usajili na Upimaji wa Mbio za Kimataifa (AMIS) kwa kushirikiana na Shirikisho la Kimataifa la Mchezo wa Riadha (World Athletics).

"Mbio zetu sasa hivi zimeorodheshwa katika tovuti ya mbio za kimataifa ya AIMS. Huko ndipo wakimbiaji wengi wa kimataifa wamekuwa wakiziona na kuvutiwa na kujitoa kwetu kuhamasisha jamii kuchangia gharama za upasuaji kwa watoto wenye matatizo ya moyo, ujenzi wa kituo cha mawasiliano katika Hospitali ya Ocean Road na kuchangia katika utunzaji wa mazingira kupitia kampeni yetu ya 'Pendezesha Tanzania'," alisema Nsekela.

Kuhusu maandalizi ya mbio hizo zitakazofanyika Jumapili ya Agosti 15, mwaka huu, Nsekela alisema yamefikia hatua nzuri na kuahidi washiriki wote kupata uzoefu wa kimataifa. Alisema wataalamu wa usimamizi wa mbio za kimataifa kutoka Shirikisho la Kimataifa la Mchezo wa Riadha wanatarajiwa kufika nchini mapema wiki ijayo, kwa ajili ya maandalizi ya mwisho.

Katika mkutano huo na waandishi wa habari, Benki ya CRDB pia ilitambulisha vifaa vitakavyotumika mwaka huu ikiwamo medali, fulana, bib, mfuko wa kuwekea vifaa (back-pack).

Aidha, Nsekela alitumia fursa hiyo kuweka hadharani jina la mgeni rasmi katika mbio hizo, ambaye anategemewa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, huku akiongezea kuwa viongozi mbalimbali wanatarajiwa kushiriki mbio hizo ikiwamo Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania, Tulia Ackson ambaye ataambatana na wabunge, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, pamoja na viongozi wengine mbalimbali wa serikali.

"Nitumie fursa hii kipekee kabisa kumshukuru sana Waziri Mkuu kwa kukubali kuwa mgeni rasmi siku hiyo. Amenitumia salamu kuwa yeye muda huu uliobaki anajifua tutakutana naye hiyo Agosti 15," alisema Nsekela.

Aliongezea kuwa tayari benki hiyo imeshapata muongozo wa Jeshi la Polisi kuhusu kuhakikisha usalama siku hiyo, na kulishukuru jeshi hilo kwa ushirikiano mkubwa, ambao wamewapatia.

Katika siku hizi chache zilizobaki, Nsekela amewataka Watanzania kuendelea kujisajili CRDB Bank Marathon kwani pamoja na kuwa mbio hizo sasa hivi ni za kimataifa, lengo kubwa ni kukuza uzalendo miongoni mwa Watanzania kwa kuwaleta pamoja kutatua changamoto katika jamii.

"Tungependa zaidi kuona Watanzania wakishiriki kwa wingi kwani hii ni marathon yetu na tungependa pia kuona zawadi hizi zikibaki nyumbani," aliongezea.

Akizungumza kwa niaba ya kampuni shirika wa CRDB Bank Maratho, Mkurugenzi wa Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Sanlam, Julius Magabe, alisema kampuni yao inajivunia kuwa washirika wa CRDB Bank Marathon kutokana na mbio hizo kujikita zaidi katika kuhamasisha watu kusaidia jamii.

Mbali na mashindano ya mbio siku hiyo, pia kutakuwa na burudani za ngoma za asili kutoka mikoa mbalimbali, wakiwamo wasanii Ben Pol, Mimi Marz, Dullah Makabila na MC Kinata, burudani kutoka wasanii wa kimataifa pamoja na burudani ya vyakula na vinywaji.

**MEDALI...**




Hansle Parchment raia wa Jamaica, akishangilia kwa furaha baada ya kutwaa Medali ya Dhahabu katika mbio za kuruka vihunzi mita 110 akimpiku Mmarekani Grant Holloway kwenye michuano ya Olimpiki inayoendelea nchini Japan. **PICHA: MTANDAO**

# Mwenda aipeleka KMC Ndondo Cup

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Habibu Kondo, amesema kwa sasa wanafuatilia michuano inayoendelea nchini hasa Ndondo Cup, kuhakikisha wanapata warithi wa David Raphael na Israel Mwenda, ambao hawatakuwa sehemu ya kikosi chao msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/22.

Raphael anayecheza nafasi ya beki wa kushoto, amesaini mkataba wa miaka miwili na Yanga wakati Mwenda naye inaelezwa tayari amemalizana na Simba kwa kusaini mkataba wa miaka mitatu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kondo alisema kwa sasa yupo katika mipango ya kuboresha kikosi cha timu hiyo kwa kutafuta warithi wa nyota hao wawili, ambao hawatakuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao.

Alisema wanaangalia zaidi wachezaji wazawa na kujikita zaidi katika michuano ya Ndondo Cup, kwa ajili ya kupata wachezaji, ambao wataleta ushindani na kusaidia timu hiyo katika michezo ya ligi hiyo.

"Tunawapa kipaumbele wachezaji wazawa, kabla ya kuangalia wachezaji wa timu za Ligi Kuu, na kwanza tumejikita zaidi michuano ya Ndondo Cup kuangalia nyota wazuri na kusaidia timu kufikia malengo kwa msimu mpya wa ligi," alisema.

Alisema ana imani katika timu zinazoshiriki Ndondo Cup, zinakuwa na wachezaji wazuri wanaoweza kuisaidia timu hiyo, kama watakuwa makini kuhakikisha wanapata mchezaji sahihi anayeweza kuisaidia timu hiyo.

"Bado hatujajua kwamba huku chini kuna wachezaji wazuri. Licha ya kupeleka mapendekezo yangu kwa uongozi, pia nimekuwa makini kufuatilia Ndondo Cup, wapo nyota wazuri, mfano, Iddi Selemani 'Nado', ambaye alitokea katika Ndondo Cup na kusajiliwa na Mbeya City na baadaye kwenda Azam FC," alisema Kondo.

## Shikalo bado ana mkataba - Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema golikipa wake namba moja kwa sasa, Farouk Shikalo bado ana mkataba na klabu hiyo, tofauti na uvumi unaoenezwa kuwa anacheza, bila ya kuwa na mkataba wowote.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa ameeleza kushangazwa na taarifa hizo na kusema kuwa huo ni uzushi mtupu na inafaa upuuzwe.

Hivi karibuni zilizuka tetesi kuwa, kipa huyo amemaliza mkataba na klabu ya Yanga na anacheza mechi bila ya kuwa na mkataba wowote, hauli hiyo ikija baada ya juzi Jumatano kipa huyo raia wa Kenya, kusimama golini wakati Yanga ikitoka sare na Atlabara ya Sudan Kusini, kwenye mechi ya Kombe la Kagame linaloendelea kutimua vumbi nchini.

"Huo ni uzushi. Huwezi kumtumikisha mchezaji bila mkataba. Ni mwajiriwa wa klabu ya Yanga na ana mkataba mpaka sasa na ndiyo maana anacheza. Shikalo siyo mtoto mdogo na hawezi kufanya kazi huku mkataba ukiwa umekwisha," alisema Katibu huyo.

Yanga ilimsajili kipa huyo mwaka 2019, kutoka Bandari ya Kenya na amekuwa akicheza kwa kupokezana na Metacha Mnata kwa nyakati tofauti.

## Harerimana kuibukia Mbeya Kwanza FC

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbeya Kwanza FC itakayoanza kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu unaotarajiwa kuanza Septemba 25, mwaka huu, upo katika mazungumzo na aliyekuwa Kocha Mkuu wa KMC FC, raia wa Burundi, Haruna Harerimana, ili kukinoa kikosi cha timu hiyo.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, kutoka kwa mtu wa karibu na kocha huyo, zimeeleza tayari mwalimu huyo yupo hapa nchini kwa mazungumzo na mmoja wa viongozi wa timu hiyo na mambo yakienda vizuri pande zote mbii wataingia mkataba.

"Kocha yuko nchini na yupo kwenye mazungumzo na uongozi wa Mbeya Kwanza, ambayo itashiriki Ligi Kuu msimu huu mpya, kila kitu kinaenda vizuri na huenda ndani ya hizi siku tatu atasaini mkataba wa kukinoa kikosi cha timu hiyo," mtoa habari huyo alieleza.

Gazeti hili lilimtafuta Mwenyekiti wa Mbeya Kwanza, Mohammed Mashango, ambaye hata hivyo hakutaka kufunguka juu ya raia huyo wa Burundi kufanya naye mazungumzo zaidi ya kueleza kwa ufupi "tupo katika maboresho ya benchi letu la ufundi".

# Michezo

Ijumaa Agosti 6, 2021

Nipashe






## Grealish aweka rekodi akitua City

HABARI UK. 22

PAMBANA...




Winga mpya wa timu ya Yanga, Jimmy Ukonde (kushoto), akipambana kumiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Atlabara ya Sudan Kusini katika mchezo wa michuano ya Cecafa Kagame Cup, uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na timu hizo kutoka suluhu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga na mikakati CAF

**Na Saada Akida**

MKURUGENZI wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Thabiti Kandoro, amesema wamejipangaa vizuri kuhakikisha wanakuwa na mechi nyingi za ushindani za kirafiki za kimataifa kwa ajili ya maandalizi kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo inatarajia kuanza mapema Septemba 10, mwaka huu.

Kikosi cha Yanga kinatarajiwa kuingia kambini Agosti 15, mwaka huu baada ya wachezaji wapya kuungana na wengine katika kambi yao iliyopo Kigamboni na baadaye kwenda nchini Morocco ambapo kitaweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kandoro alisema maamuzi hayo ya kutafuta mechi nyingi za kirafiki za ushindani ni baada ya kuona ratiba kuwa ngumu huku wakielekea kushiriki michuano ya kimataifa wakati ambao Ligi Kuu Tanzania Bara itakuwa haijaanza.

Alisema wamejipanga vizuri kutafuta mechi nyingi za ushindani za kirafiki ambazo zitasaidia timu yao kujiandaa na michuano ya kimataifa ambayo kwa muda mrefu hawajashiriki huku sasa wakitaka kufanya vizuri.

"Ni kweli tumeona ratiba ya Ligi Kuu kuanza Septemba 29, mwaka huu huku michuano ya kimataifa nayo inaanza mapema. Tumeona hilo na sasa tayari tumeanza kutafuta timu za ushindani ambazo tutacheza mechi za kirafiki ikiwamo siku ya Wananchi, pia timu itaenda nje ya nchi kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya," alisema Kandoro.

Kuhusu usajili mpya, alisema: "Tumejipanga vizuri, mashabiki wanatakiwa kutulia na viongozi tunaendelea na mchakato wa usajili wa wachezaji wapya na wengine tunaona wanaendelea katika michuano ya Kagame na kufanya vizuri akiwamo Jimmy Ukonde.

# CHAMA ATANGAZA KUONDOKA SIMBA

## Amtaja Miquissone, awataka mashabiki kumwelewa, asema atazungumza na klabu na kuiomba kumruhusu kama...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI winga wa Simba, Luis Miquissone, akijiandaa kujiunga na mabingwa wa Afrika mara mbili mfululizo, Al Ahly ya Misri, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Mzambia Clatous Chama, naye ameshusha kishindo kizito baada ya kueleza kuwa anasikilizia ofa nono kutua mezani.

Ubora aliouonyesha Miquissone katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliomalizika kwa Al Ahly kuibuka mabingwa, hususan kwenye michezo miwili nyumbani na ugenini dhidi ya Wamisri hao, imeifanya miamba hiyo kutoa ofa nono ambayo inaelezwa imekuwa vigumu Simba kuikataa.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka vyombo mbalimbali vya habari vya Misri, klabu hiyo imekubali kutoa dola za Marekani 900,000 zaidi ya Sh. bilioni mbili za Tanzania ofa ambayo imekubaliwa na Simba kumuuza Miquissone.

Hata hivyo, Simba bado haijatangaza rasmi uamuzi huo wa kumuuza Miquissone, lakini inaelezwa ni suala la muda tu kwa kuwa winga huyo tayari amewaaga marafiki zake wa karibu kuwa anajiunga na Al Ahly.

Lakini Chama akizungumzia taarifa za kuwapo uwezekano wa kuondoka kwa Miquissone, alisema hata yeye kama itakuja ofa nono mezani atakaa na klabu yake hiyo kuiomba umuuze.

"Kama Miquissone akiondoka, mimi pia ikija ofa nzuri klabu ikakubali nitaondoka. Nimekaa Simba miaka mitatu, nimefanya mambo mazuri, mashabiki wajue kuwa haya ni mambo ya kawaida yanatokea.

"Nilishasema tangu awali kama muda ukifika na mimi nitaondoka endapo ofa itakuja na Simba ikikubali," alisema.

Chama ambaye amekuwa na mchango mkubwa kwa klabu hiyo tangu ajiunge nayo mwaka 2018, aliongeza: "Ukitazama miaka yangu mitatu hapa Tanzania, nadhani nimefanya vizuri kwa timu, ninauhakika mashabiki wanapaswa kuelewa, endapo kuna klabu kubwa itajitokeza tutakaa na kujadili tukikubaliana na Simba ikikubali nitaondoka."

Kwa misimu yote mitatu ambayo ameichezea Simba, Chama ameiwezesha klabu hiyo kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu mara tatu, huku ikibeba Kombe la FA mara mbili mfululizo na kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mara mbili.

Tayari Simba ipo katika mipango ya kuboresha kikosi chake na imeshatangaza usajili wa wachezaji wawili, winga Mmalawi Peter Banda pamoja na mshambuliaji Yusuph Mhilu kutoka Kagera Sugar.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alimwambia mwandishi wetu kuwa, bado wataendelea kutangaza usajili mpya kwa ajili ya kukiimarisha kikosi hicho kwa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na ile ya ndani.

"Kwa sasa kazi yetu ni moja tu, kutangaza usajili, mambo mengine tunayaweka kando kwanza," alisema.

Michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika inatarajiwa kuanza Septemba 10, mwaka huu huku Tanzania Bara ikiwakilishwa na Simba na Yanga, wakati Kombe la Shirikisho Afrika jukumu hilo likibaki kwa Azam FC na Kagera Sugar.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >